**TCU** yafungua dirisha kujaza nafasi 56,970

UKURASA 2



**BITEKO** atoa maagizo ya kukabiliana na El Nino

UKURASA 5



**ALIYESHINDA** mashauri 26 adaiwa kuwa ni wakili feki

UKURASA 17



SUPA JACKPOT
TZS.1,161,795,478
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Nipashe
Jumamosi Oktoba 14, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581463
www.ippmedia.com
LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

# Spika Tulia atoa neno wanaotemwa na Rais

**WADAU** watoa maoni, wabainisha kiini cha utenguzi... *Endelea ukurasa wa 2*



**'Viongozi wengi ambao uteuzi wao unatenguliwa na Rais, sababu kubwa ni kwamba wanakuwa hawana maandalizi ya uongozi."**
**Dk. Tulia.**



**Kauli ya Spika ni sahihi na kwamba mifumo mibovu iliyopo inachangia hilo. Zamani wanaoteuliwa walikuwa wanapatiwa mafunzo kwa ajili ya kuwafunda lakini sasa hayapo."**
**Prof. Semboja.**



**'Kinachosababisha kuwapo kwa uteuzi na utenguzi ni kwamba mifumo haifanyi kazi inavyostahili. Mtu achunguzwe kabla hajapewa nafasi kama anakidhi vigezo."**
**Mnyika.**



## KUMBUKIZI MIAKA 24:
# Kimiti asimulia Mwalimu Nyerere alivyonusuru Muungano kuvunjika

Paul Kimiti

UKURASA 4, 9, 10, 11, 12, 13 ,14, 15 & 16

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### MABASI YAPELEKA LATRA OMBI KUPANDISHA NAULI

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imepokea maombi kutoka kampuni tatu zinazotoa huduma...



UKURASA WA 24

### STARS YAPEWA NAFASI AFCON

BAADA ya ratiba ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika...



## Israel yaamuru watu kuondoka Gaza saa 24

UKURASA 17

**MICHEZO** SIMBA SC, YANGA ZACHANGA KARATA UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Rais Dk Samia Suluhu Hassan (kulia), akifanya mazungumzo na Mwanzilishi na Mwenyekiti wa Bharti Enterprises, Sunil Bharti Mittal (wa tatu kushoto) na ujumbe wake. Rais Samia alikutana na Bharti Enterprises wakati wa ziara yake ya kiserikali ya siku nne hivi majuzi nchini India. Bharti inaendesha Airtel Tanzania kwa asilimia 49 ya hisa zinazomilikiwa na serikali ya Tanzania. **NA MPIGAPICHA WETU.**

# Spika Tulia atoa neno wanaotemwa na Rais

**Na Waandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema viongozi ambao uteuzi wao unatenguliwa na Rais, sababu kubwa ni kwamba wanakuwa hawana maandalizi ya uongozi.

Kutokana na kauli hiyo, wadau mbalimbali wameibuka na kutoa maoni yao.

Katika mdahalo wa Wiki ya Vijana ulioandaliwa mjini Babati jana, Dk. Tulia alisema watu wanatemwa kutokana na kukosa maandalizi ya kuwa viongozi na kugombea ni sehemu ya maandalizi.

"Ukifanya maandalizi ya uongozi nafasi zinakukuta ukiwa tayari na kuna maandalizi ya elimu na maadili. Gombea ili watu wakuone unazungumzaje na unajielezaje ili watu wakuchague,"alisema.

Dk. Tulia alisema kuna mazingira ukivaa suruali unaonekana huna maadili na yako mengine mtu anaonekana wa kawaida na kuchukuliwa tofauti.

Aliwataka vijana wajiangalie wanavyokuwa wanajibu mitandaoni jamii inawaonaje.

Waziri wa Nchi, Sera na Uratibu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hamza Hassan Juma, alisema kijana inabidi ajiandae kupata viongozi kwa kufanya maandalizi.

Alisema Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, angekuwa mchoyo angewaacha Wazanzibari waendelee kutawaliwa na wakoloni.

**CHADEMA YAFUNGUKA**

Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, akitoa maoni yake kuhusiana na kauli ya Spika Tulia, alisema kinachosababisha kuwapo kwa uteuzi na utenguzi ni mifumo haifanyi kazi inavyostahili.

"Kabla ya kiongozi kuteuliwa mfumo wa kuhakiki viongozi ambao unatakiwa kuzishauri mamlaka za uteuzi kama mteuliwa anakidhi vigezo," alisema.

Mnyika alisema pamoja na kwamba kuna changamoto ya maandalizi ya uteuzi, kwa nafasi zilizopo za uteuzi, wako viongozi wa kuziba isipokuwa mifumo ndiyo haioni viongozi mwafaka kwa kuwapima. Alisema mifumo imekuwa ikimgundua mtu ana tatizo wakati ameshakabidhiwa nafasi.

"Ufumbuzi wa muda mrefu kwa ajili ya kusaidia ni Katiba Mpya ambayo itapunguza mamlaka Rais ya kuteua watu wengi ambao hawajui.

"Mamlaka ya uteuzi itateua baadhi na walio wengi watateuliwa na mamlaka ambazo zinawafahamu. Pia mamlaka ikiteua kunakuwa na kuthibitisha mtu kwenye kuteuliwa, anapimwa uwezo wake kabla ya kuanza kazi, kama ana makando kando hayasubiri mpaka aanze kazi.

"Katika kipindi hiki cha mpito, kuna vyombo ndani ya serikali vikifanya kazi inavyotakiwa. Mfano Idara ya Usalama wa Taifa ina wajibu wa kutoa taarifa kwa mamlaka kuhusu mtu yeyote anayependekezwa kuteuliwa katika nafasi fulani. Ifanye kazi yake ya uchunguzi vizuri zaidi," alisema.

Alisema vyombo vingine vinavyohusika na utumishi wa umma navyo kabla ya mtu kuteuliwa viwe na uwezo wa kutoa maoni kwa sababu wanawatambua watumishi wao na kusisitiza kuwa kwenye mahakama kuna Tume ya Utumishi wa Mahakama nayo ipewe huo wajibu na kazi ya kutoa maoni.

Mchambuzi wa Masuala ya Uchumi, Prof. Haji Semboja, alisema kauli ya Spika ni sahihi na kwamba mifumo mibovu iliyopo inachangia hilo alilolieleza.

Alisema mfumo mzima serikalini unapaswa kutambua kuwa, serikali ni taasisi ambayo inahitajika kuwa na watu wenye elimu, maarifa, ujuzi, uelewa na utashi.

Prof. Semboja alikumbusha kuwa mwaka 1960 hadi 1970 viongozi wengi waliokuwa wanafanya kazi serikalini walipelekwa katika shule mbalimbali na kufundishwa na kupatiwa elimu ya utumishi ndani ya serikali.

Alisema mafunzo hayo yalikuwa yanatolewa kwa ajili ya kuwafunda au kuwatayarisha watu kuwa na mtazamo wa kufanya kazi za kuwatumikia wananchi.

"Hapa katikati ndipo tulipoharibu. Kwanza, hivi vyuo vya mafunzo walivibadilisha na kuanza kutoa mafunzo mengine ambayo si hayo yaliyokusudiwa," alisema

Mchambuzi huyo alisema kwa kuwa, mtu huyo hajafundishwa wala kufundwa inakuwa ni kosa kubwa la jinai na serikali inayowatendea wananchi wake.

"Hivi vyuo wameviua kuna utashi fulani binadamu anaufanya bila kujua anawakosea wengine. Jambo la pili katika mabadiliko ambayo tunayatengeneza tulifikiri wafanyakazi wa sekta binafsi ambao hawana elimu ya masuala ya serikali kuwaajiri bila kuwapatia mafunzo ni kosa namba mbili.

"Huwezi kumtoa mtu kwenye sekta ambayo hana utashi nayo. Hakujitayarisha, hana elimu nayo na kumwambia nenda katoe huduma kule. Hili ni kosa la mifumo si kosa binafsi bali ni mfumo umeharibu," alisema.

Semboja alisema mtu atapanda ngazi akiwa amefanya mambo mawili katika nafasi yake ya kazi ikiwamo kupata elimu husika katika eneo analofanyia kazi.

Alisema watu wanapanda vyeo bila kuangalia taratibu muhimu na kujikuta wanapeana ulaji bila kuangalia utendaji wake wa kazi.

**IMEANDALIWA na Jaliwason Jasson (BABATI), Romana Mallya na Beatrice Shayo (DAR)**

# TCU yafungua dirisha kujaza nafasi 56,970

**Na Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) imefungua awamu ya mwisho ya udahili wa Shahada kwa mwaka wa masomo 2023/24 huku ikitoa wito kwa waombaji wanaostahili kutuma maombi kwa kuwa nafasi 56,968 bado hazijajazwa.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, aliwataka waliokosa katika awamu tatu zilizopita, kutuma maombi yao katika vyuo husika kwa kuangalia kozi zinazowafaa.

"Kwa ujumla tuna nafasi za vyuo vikuu 187,084 kwa mwaka huu, katika madirisha matatu yaliyopita, jumla ya waombaji 130,116 wameandikishwa, hivyo tunawakaribisha wale ambao bado watumie dirisha hili la nne," alisema.

Prof. Kipampa alisema awamu ya nne na ya mwisho imeanza jana (Oktoba 13) hadi Oktoba 24, mwaka huu.

"Tume imepokea maombi kutoka kwa wadau mbalimbali wanaomba kuongezewa muda wa udahili ili kuwapa wale ambao hawakuweza kupokelewa au kuomba udahili kufanya hivyo," alisema.

Alivitaka vyuo vikuu ambavyo bado vina fursa basi waruhusu wanaohitaji kutuma maombi, wafanye vivyo na kusisitiza kuwa dirisha hilo ni la mwisho.

Prof. Kihampa aliwataka waombaji na waliojiunga na vyuo zaidi ya kimoja, kuhakikisha wanathibitisha chuo kimoja pekee ifikapo Oktoba 25, mwaka huu. "Oktoba 21 na 22, vyuo vikuu vitatakiwa kuwasilisha orodha ya watahiniwa ambao wamesajiliwa katika taasisi zao na Oktoba 25, mwaka huu, vyuo vikuu vitatangaza majina ya walioandikishwa na wale waliothibitishwa kusajiliwa," alisema.

Prof. Kihampa amewaonya waombaji na wananchi kwa ujumla kuepuka kupotoshwa na watu wasio waaminifu wanaodai kutoa huduma za namna ya kujiunga na vyuo vya elimu ya juu nchini.

HABARI KITAIFA



Ofisa jinsia, Wanawake, Vijana na Watoto wa Shirika linalojihusisha na masuala ya watu wenye ulemavu la Foundation For Disabilities Hope (FDH), Halima Msofe akizungumza juzi na wanafunzi wa kike wa shule ya msingi Buigiri wasioona wilayani Chamwino mkoani Dodoma kuhusu umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Mtaalamu alia uhaba wataalam mishipa fahamu, ongezeko vifo

**Na Romana Mallya**

TAKWIMU zinaonyesha Tanzania ina wataalamu wa mishipa ya fahamu wapatao 14 tu hali ambayo inachangia kuwapo kwa wagonjwa wengi na ongezeko la vifo vitokanavyo na magonjwa hayo.

Mwenyekiti wa Chama cha Wanasayansi wa Magonjwa ya Mishipa ya Fahamu Tanzania (TNA) na Profesa wa Magonjwa ya Mishipa ya Fahamu, William Matuja, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Alisema kati ya wataalam hao, 11 ni wa upande wa watu wazima na watatu kwa ajili ya watoto. Alisema idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya Watanzania kwa sasa.

Prof. Matuja aliyasema hayo wakati akizungumzia kuhusu kongamano la kimataifa la 14 katika Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara lililoandaliwa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) pamoja nao ili kutoa mafunzo ya kukabiliana na magonjwa ya mishipa ya fahamu.

Alitaja magonjwa yanayotokana na mishipa kuwa ni kiharusi, kifafa, maambukizi kwenye mishipa ya fahamu, magonjwa ya dharura ya mishipa ammbayo aslisema hata katika bara zima la Afrika kuna wataalamu wachache.

"Takwimu za Tanzania zinaonyesha kuna wataalamu wa mishipa ya fahamu 14 tu ambapo kati yao, 11 ni wa upande wa watu wazima na wa watatu ni wa wa watoto, ikiwa ni idadi ndogo ukilinganisha na idadi ya Watanzania kwa sasa," alisema.

Prof. Matuja alisema kongamano hilo litafanyika kwa siku nne kuanzia Oktoba 28 Muhimbili-Mlonganzila na uhudhuriwa na washiriki 150 kutoka hospitali za mikoa yote.

Alisema kuwa washiriki wengine watatoka nchi 20 barani Afrika ikiwamo Angola, Benin, Burkina Faso, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Ethiopia, Gabon, Ghana, Ivory Coast, Kenya, Madagascar, Mali, Mozambique, Niger, Nigeria, South Africa, Senegal, Togo, Uganda, Zambia na Zimbabwe.

Prof. Matuja alisema magonjwa ya mishipa ya fahamu na vifo vinavyoambatana nayo yanazidi kuongezeka siku hadi siku.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), inakadiriwa kuwa kila sekunde 40 binadamu mmoja hukumbwa na ugonjwa wa kiharusi na kila sekunde tatu 3.5 kifo hutokea kutokana na ugonjwa huo. Prof. Matuja amesema, mojawapo ya mkakati wa kukabiliana na uhaba wa wataalamu ni pamoja na kuwapatia mafunzo madaktari na wataalamu wengine ili kuweza kutambua na kutibu magonjwa ya mishipa ya fahamu.

Alisema juhudi hizo zitasaidia madaktari wakirejea kwenye maeneo yao ya kazi waweze kuwapatia huduma wagonjwa wa namna hiyo kwa ufanisi zaidi.

Katika kongamano hilo kutakuwa na wazungumzaji kutoka vyama tisa vya magonjwa ya mishipa ya fahamu vya kimataifa kutoka mabara ya Ulaya, Afrika na Marekani.

Wataalam hao watashirikiana na wakufunzi kutoka TNA katika kutoa mafunzo hayo. Mashirika hayo ni pamoja na (EAN, AFAN, AAN, IBRO, IHS, ILAE, MDS PAUNS na WFN).

# Mabasi yapeleka LATRA ombi kupandisha nauli

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imepokea ombi kutoka kampuni tatu zinazotoa huduma ya usafiri wa abiria wa masafa marefu kufanya marejeo ya nauli za mabasi kutokana na ongezeko la gharama za uendeshaji.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano cha LATRA, kampuni hizo ni Super Feo Enterprises, ABC Upper Class and Transportation Ltd na Happy Nation Co. Ltd.

Taarifa hiyo ilisema kuwa kampuni hizo zimeomba LATRA kufanya marejeo ya nauli za mabasi huku zikitaja sababu nyingine kuwa ni kupanda kwa bei ya mafuta (petroli na dizeli).

"Mapendekezo ya kampuni hizo ni kuongeza nauli ya sasa ya Sh. 56.88 kwa kilometa moja kwa kila abiria. Super Feo Enterprises kwa daraja la kati nauli pendekezwa kwa kilometa moja kwa kila abiria imeomba iwe Sh. 101.88 na ongezeko kwa kilometa moja kwa kila abiria iwe Sh. 45 sawa na asilimia 79.11," ilisema.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa ABC Upper Class and Transportation imependekeza kwa daraja la kati nauli kwa kilometa moja kwa kila abiria iwe Sh. 92.84 ongezeko kwa kilometa moja kwa kila abiria iwe Sh. 36.96 sawa na asilimia 63.22.

Aidha, ilisema Happy Nation Co. Ltd kwa daraja la kati nauli pendekezwa kwa kilometa moja kwa kila abiria ni 84.06 na ongezeko kwa kilometa moja kwa kila abiria Sh. 27.18 sawa na 47.78.

"Kwa kuzingatia kifungu cha 21 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413 pamoja na kanuni ya 9(3) ya Kanuni za LATRA (Tozo) za Mwaka 2020 (Tangazo la Serikali Na. 82 la tarehe 7/2/2020), mamlaka inapaswa kutoa fursa kwa kampuni hizi kuwasilisha mapendekezo yao kwa wadau wa usafiri wa abiria kisha kukusanya maoni ya wadau kabla ya kufikia uamuzi wa kufanya marejeo ya nauli zilizotumika," ilisema taarifa hiyo.

Pia taarifa ilisema nauli zinazotumika kwa sasa zilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 18 la tarehe 6 Mei, 2022.

Taarifa hiyo ilisema kutokana na maombi hayo, mamlaka imeandaa mkutano wa wadau kupokea maoni utakaofanyika Oktoba 18, mwaka huu, katika ukumbi wa Arnaoutouglou, Dar es Salaam kuanzia saa 3:00 asubuhi.

Aidha, taarifa ilisema LATRA itawasilisha mapendekezo ya vigezo vya mchakato wa kuridhia mapitio ya viwango vya nauli za mabasi yanayotoa huduma mijini (daladala). "Wasilisho la LATRA litafanywa kwa mujibu wa kanuni ya 13 ya Kanuni za LATRA (Tozo) za Mwaka 2020 (Tangazo la Serikali. Na. 82 la tarehe 7/2/2020).

"Kutokana na umuhimu wa suala hili, LATRA inawaalika wadau wote wa usafiri wa umma na wananchi kwa ujumla kuhudhuria mkutano huu muhimu ili kutoa maoni baada ya kusikiliza mapendekezo yatakayowasilishwa na kampuni zilizoleta maombi ," ilisema.

# Mfanyabiashara akutwa amefariki ndani ya gari lake

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MFANYABIASHARA mkubwa jijini Arusha, aliyejulikana kwa jina moja la Mallya, amekutwa amefariki dunia ndani ya gari lake aina ya Suzuki Escudo na mwili wake kubainika baada ya harufu kali kusikika.

Mwili huo umekutwa katika gari lenye namba za usajili T 466 AUB lililokuwa limeegeshwa katika eneo la Kaloleni jijini Arusha.

Mashuhuda wa tukio hilo walisema mwili wa mfanyabiashara huyo uligundulika kuwapo kwenye gari hilo baada waosha magari eneo hilo kusikia harufu kali ikitokea kwenye gari hilo jana asubuhi na ndipo polisi walipofika.

Walisema mfanyabiashara huyo amekuwa na tabia ya kufika eneo hilo na kuegesha gari lake kisha kwenda baa iliyoko eneo hilo kwa ajili ya kula chakula na kunywa.

Mwenyekiti wa eneo hilo, maarufu kwa wauzaji wa magari (madalali), Alex Kahela, alisema alipata taarifa jana kuhusiana na tukio hilo na baada ya kufika, aliitambua gari hilo kuwa ni mali ya mfanyabiashara huyo.

"Nilifika eneo la tukio na kujaribu kuchungulia ndani ya gari baada ya milango kufungwa ndipo tulipomuona mzee Malya. Hatufahamu chanzo cha kifo chake. Kwa makadirio gari litakuwa limekaa hapa kwa siku mbili au tatu," alisema.

Mwosha magari, Juma Jumapili, alisema juzi jioni walisikia harufu hata hivyo, haikuwa kali sana na kujikuta wakiendelea na shughuli zao na ndipo jana walibaini imeongezeka.

Shuhuda mwingine, Peter Kivuyo, alisema wamemtambua kuwa ni Mzee Malya na pembeni ya mwili wake, kukiwa na mabunda ya fedha na michirizi ya damu eneo la kifua.

"Niliuona mwili wa marehemu sehemu ya kifua kukiwa na michirizi ya damu huku pembeni akionekana ameshika mabunda ya fedha," alisema Kivuyo.

Kamanda wa Polisi mkoani Arusha, Justine Masejo, hapatikana kuongelea tukio hilo na gari la marehemu li?iwa na mwili lilichukuliwa kwa kuvutwa na kupelekwa chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Arusha kwa ajili ya uchunguzi zaidi.



# Kimiti asimulia Mwalimu Nyerere alivyonusuru Muungano kuvunjika

**Na Mwandishi Wetu**

MIAKA 24 imetimia tangu mwasisi wa taifa la Tanganyika na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, alipofariki dunia katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas , London nchini Uingereza alikokuwa akipatiwa matibabu.

Kuondoka kwa kiongozi huyo aliyejitolea kwa moyo wote kupigania ukombozi wa taifa hili kujitawala kutoka katika makucha ya wakoloni, lilikuwa pigo kwa Tanzania.

Pia Afrika na dunia nzima iliomboleza ndiyo maana mazishi yake yalikuwa makubwa na yalivuta watu wengi.

Wakati leo ikiwa ni kumbukumbu ya kifo chake, jina la Nyerere limekuwa katika akili na mioyo ya watu kutokana na ama kufanya kazi naye alipokuwa Rais wa nchi au mwenyekiti wa chama tawala TANU na baadaye Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Miongoni mwa watu ambao bado wana kumbukumbu ya mambo kadhaa yaliyofanywa na Nyerere ni Paul Kimiti ambaye alishika nafasi mbalimbali zikiwamo uwaziri, ujumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, ubunge na ukuu wa mkoa.

Kimiti alitumika katika nafasi hizo kwa awamu tofauti kuanzia awamu ya kwanza chini ya Nyerere hadi awamu ya tatu, Benjamin Mkapa akiwa Rais na mwenyekiti wa CCM.

Yako mengi ambayo mwanasiasa huyo mkongwe anayakumbuka lakini kubwa zaidi ni tukio la mwaka 1993 lililoibuka bungeni (wakati huo vikao vya Bunge la Bajeti vikifanyikia Karimjee, Dar es Salaam).

Tukio hilo ni la kuibuka kwa kundi la wabunge 55, maarufu kama G-55. Kundi hilo liliundwa na wabunge waliokuwa machachari wakati huo wakiongozwa na Njelu Kasaka (marehemu) aliyekuwa Mbunge wa Chunya na baadaye Lupa mkoani Mbeya.

Wabunge hao waliibua hoja ya kutaka kuundwa kwa serikali ya Tanganyika na waliwasilisha hoja bungeni kuhusu azma hiyo huku wakitia saini kuwa wanataka mchakato huo kufanyika haraka.



Paul Kimiti

Mbali na Kasaka, wabunge wengine walikuwa Lumuli Kasyupa, William Mpiluka, Mateo Qaresi, Jared Ghachocha, Dk. Mganga Ole Kipuyo, Philip Marmo, Arcado Ntagazwa, Patrick Qorro, Japhet Sichone, Jenerali Ulimwengu, Abel Mwanga, Prof Aron Massawe, Shashu Lugeye na Sebastian Kinyondo.

Wengine ni Phares Kabuye, Mbwete Hombee, Kisyeri Chambiri, John Byeitima, Mussa Nkhangaa, Abdallah Saidi Nakuwa, Edward Ayila, Dk. Ndembwela Ngunangwa, Mathias Kihaule, Adamu karumbeta, halimenshi Mayonga, Dk. John Katunzi, Ismail Iwvata, Tobi Mweri, Aidan Livigha, Tabitha Siwale, Obel Mwamfupe, Othman Mpakani, Evarist Mwanansao, Paschal Degera, Erasto Losioki, Charles Kagonji, Nassoro Malocho, Venance Ngula na Benedict Losurutia.

Katika kundi hilo walikuwapo pia Dk. Degratius Mwita, Phineas Nnko, John Mwanga, Chadiel Mgonja, Guntram Itatiro, Paschal Mabiti, Edith Munuo, Luteni Kanali John Mhina, Raphael Shempemba, Balozi George Nhigula, Christian Fundisha, Samuel Kinuno, Rajab Kombo, Samuel Luangisa na Maria Kamm.

**KUMBUKUMBU YA KIMITI**

Akizungumza katika mahojiano maalum nyumbani kwake, Dar es Salaam, hivi karibuni Kimiti alisema kipindi hicho kilikuwa cha mtikisiko kwa taifa na baadhi ya Watanzania waligawanyika na kutokuwa na uhakika kuhusu nini kitatokea.

Kwa mujibu wa Kimiti, kundi hilo la G55 lilikuwa na hoja kuu ya kutaka iundwe serikali ya Tanganyika na iwe na madaraka kamili kama Zanzibar, hivyo kuwe na serikali tatu badala ya muundo wa serikali mbili ulioanza mwaka 1964 baada ya Zanzibar na Tanganyika kuungana na kuanzishwa kwa taifa la Tanzania.

"Kwa asiyejua faida za Muungano alitaka iwe hivyo lakini hawakujua athari gani zingetokea kama mchakato ungefanyika na hatimaye azma hiyo kutimia. Kwa kweli wengi hawakujua mpaka Nyerere alipokuja kulisemea. Aliitisha NEC na kueleza athari zake," alisema.

Kimiti alibainisha kuwa katika mkutano huo wa NEC uliofanyika Dodoma, Nyerere aliweka wazi kwamba kuwapo kwa serikali tatu ilimaanisha kuvunjika kwa Muungano kwa kuwa Zanzibar ingebaki peke yake na Tanganyika ingebaki peke yake.

"Nyerere alikwenda mbali zaidi aliposema baada ya kuvunjika kwa Muungano, dhambi hiyo yas ubaguzi ingeendelea kwa Zanzibar pia kutengana kwa misingi ya Pemba na Unguja.

Kwa Tanganyika pia ingekuwa hivyo. Watu wangejitambulisha kwa njia za ukabila na ukanda, hivyo Tanganyika isingekuwapo," alisema.

Mwanasiasa huyo mkongwe ambaye wakati huo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na Mbunge (wakuu wa mikoa walikuwa wabunge wa taifa kutokana na nafasi zao) alisema Nyerere katika mkutano uliofanyika Kilimani Club, Dodoma, aliweka wazi kwamba mpango wa kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika ambalo Bunge lilipitisha azimio, ulikuwa unavunja Muungano moja kwa moja, hivyo suala hilo halikubaliki. Alisema Nyerere aliendelea kulikemea mara kwa mara na hatimaye kuzimika kabisa.

**UCHAGUZI 1995**

Mwaka 1995 Tanzania ilifanya uchaguzi mkuu wa kwanza wa Rais na Wabunge uliohusisha vyama vingi vya siasa ikiwa ni takriban miaka mitatu tangu kuasisiwa kwa mfumo huo nchini, mwaka 1992.

Wakati wa vuguvugu la uchaguzi huo, Kimiti alisema Nyerere alikuwa mgeni rasmi katika moja ya sherehe za kitaifa zilizofanyikia Mbeya wakati huo yeye akiwa mkuu wa mkoa huo.

"Nakumbuka mwaka ule aliyekuwa Rais, Mzee Ali Hassan) Mwinyi, alikuwa anamaliza muda wake wa uongozi wa vipindi viwili vya urais, hivyo ilikuwa nafasi kwa wana CCM kujitokeza kwa ajili ya kuomba ridhaa ya kugombea ili kumpata mtu wa kumrithi Mwinyi. Kwa kweli wanachama wengi kiasi (walikuwa 15) walijitokeza kuchukua fomu kuomba ridhaa ya chama kuteuliwa kugombea urais ili kuchuana na wale wa kutoka vyama vingine.

"Nyerere alipofika Mbeya nakumbuka aliniuliza 'Paul kwa nini hujachukua fomu kuomba kugombea urais?' Nilimjibu kwamba kamkono kangu (uwezo) kadogo maana watu wanahonga.

Lakini kingine nilichomwambia ni kwamba nimejipima na kuona hiyo nafasi ni kubwa kwangu na nimefikiria kwenda kugombea ubunge Sumbawanga Mjini.

"Wakati ule pia alikuwapo Njelu Kasaka na bila kusita alimwuliza kwa nini amechukua fomu kugombea urais. Hakuishia hapo alimwuliza kama amefanya hivyo ili akatimize azma yake ya kuvunja Muungano kwa kuanzisha Tanganyika," alisema huku akibainisha kuwa jina la Kasaka lilikatwa mapema kama Nyerere alivyomwabia kuwa hatafanikiwa katika azma hiyo.

**•Kesho, katika mwendelezo wa mahojiano na Kimiti, anafichua alichoambiwa na Nyerere alipomteua kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.**

# Biteko atoa maagizo kukabili El Nino



**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (pichani), ameagiza kuboresha ufanisi katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Dharura wa Kuzuia na Kukabiliana na Madhara ya El Nino kama ilivyotabiriwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) Agosti 24, mwaka huu.

Dk. Biteko alitoa maelekezo hayo jana jijini hapa wakati akizindua mpango huo na kuugawa kwa mawaziri, naibu mawaziri, makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu na viongozi wa taasisi za serikali kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

Dk. Biteto alisema mpango huo umeandaliwa kuhakikisha serikali, wadau na jamii wanachukua hatua stahiki za kuzuia na kupunguza madhara yanayoweza kusababishwa na El Nino na kujiandaa kukabiliana na kurejesha hali ya madhara yatakayojitokeza.

"Ili kuwa na ufanisi katika kutekeleza mpango huu, nazielekeza sekta zote kuchukua hatua kuainisha na kuandaa rasilimali za kuzuia na kujiandaa kukabiliana na maafa endapo yatatokea kwa kila sekta kushiriki kikamilifu katika eneo lake, kutambua maeneo hatarishi yenye viashiria vya kuathirika na maafa na kuandaa mpango wa kuzuia madhara na kukabiliana na maafa, kuelimisha wananchi na kuwahimiza kuhama kwenye maeneo hatarishi, umuhimu wa kuweka akiba ya chakula na kulima mazao yanayohitaji maji mengi pamoja na hatua za kuchukua tahadhari ili kuokoa maisha yao na mali", alisema Biteko.

Maagizo mengine mengine ni kuandaa na kutekeleza mipango ya kuzuia milipuko ya magonjwa kwa binadamu, wanyama na mimea, idara na taasisi zinazohusika na mazingira na miundombinu, kuhakikisha barabara zinapitika wakati wote, kuimarisha na kusafisha mitaro na makalavati, sekta za maji, umeme na mawasiliano kuweka mipango ya kuzuia madhara na kuhakikisha uharibifu katika huduma hizo unapewa ufumbuzi mapema.

Pia aliziagiza taarifa kutolewa haraka kwa mamlaka husika yanapotokea maafa kwenye sekta na kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya maokozi na huduma za dharura pamoja na kutoa elimu kwa Watendaji katika ngazi zote ili wachukue hatua stahiki za kuzuia na kupunguza madhara ya El Nino yanayoweza kujitokeza.

Vilevile, alizitaka sekta kuimarisha na kusafisha njia za maji ya mvua na maji taka pamoja na usimamizi wa taka ngumu na uwepo wa madampo, kuimarisha madaraja na kingo za mito na mabwawa katika maeneo yote ya kimkakati, kusimamia matumizi sahihi ya mitaro na njia za maji kwa kuzuia viwanda kutiririsha uchafu katika maeneo ya makazi na sehemu za kuzalishia maji.

Kadhalika, alizitaka wizara, idara, taasisi, mikoa na halmashauri zote ziandae mipango ya utekelezaji katika maeneo yao kwa kuzingatia mpango huu uliooandaliwa na kuhakikisha mvua hizi zinatumika kwa shughuli za maendeleo.

Pia kufuatilia na kutekeleza maelekezo ya kitaalam pamoja na taarifa za utabiri wa hali ya hewa unaotolewa na TMA na kuweka utaratibu wa kuandaa ujumbe mfupi na kuusambaza kwa njia ya simu.

Biteko alisisitiza kuwa wizara zichukue wajibu wake wa kuandaa kukutana na wadau na watu walio chini yenu kuwapa maelekezo hayo na kwenye matangazo na hotuba zao kutenga eneo la kuweka ujumbe unaohusiana na kuwatahadharisha Watanzania juu ya uwepo wa madhara ya El Nino.

Akizungumza kuhusu mpango huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama amesema kuwa mara tu taarifa ya awali ya dalili za uwezekano wa uwepo wa El Nino ulipotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu imetekeleza na kuratibu hatua kadhaa za kimsingi na za awali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanawasilisha taarifa kwenye wizara na mikoa hasa mikoa husika ili kufanya tathmini ya maeneo yanayoweza kuathirika na kuandaa mipango ya hatua za kuzuia au kupunguza madhara na kujiandaa kukabiliana na maafa endapo yatatokea kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na TMA.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Ladislaus Chang'a, alishukuru serikali kwa uwekezaji mkubwa uliofanyika katika kuimarisha huduma za hali ya hewa nchini.

Alisema Ameeleza kuwa, matukio ya hali mbaya ya hewa ambayo yanaendelea kuongezeka ni pamoja na mvua kubwa za muda mfupi, joto kali, upepo mkali na vimbunga ambapo tathmini ya karibuni inaonesha matukio ya El Nino yataongezeka kwa idadi na ukubwa kadri ambavyo joto la dunia linaendelea kuongezeka.

"Mwelekeo wa mvua za vuli kwa mwaka 2023 unaonyesha msimu wa mvua za vuli utachagizwa na uwepo wa El Nino.

Tunaendelea kufanya kazi saa 24 kufuatilia mabadiliko katika bahari zote ambapo tunachokiona kwa sasa ni ukubwa wa El Nino kuwa katika nyuzi joto 1.2 ambao ni ukubwa wa wastani, na tunatarajia mvua hizo zitaenda mpaka mwezi Januari," alisema Dk. Chang'a.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba kumekucha AFL, msibweteke Yanga wautumie kuwasoma Al Ahly

**IMEBAKI** wiki moja tu kabla ya mchezo wa ufunguzi wa michuano mipya ya African Football League (AFL) kati ya wenyeji Simba dhidi ya Mabingwa wa Misri Al Ahly.

Mchezo huu ambao unatarajiwa kuvuta viongozi wengi wa soka kutoka Afrika na Duniani kwa ujumla umepangwa kuchezwa Ijumaa ijayo, Oktoba 20 ukiwa ni wa ufunguzi wa michuano hiyo mipya Afrika.

Hii ni histori kubwa inaenda kuandikwa katika kitabu cha soka hapa nchini kwa kushuhudia mchezo wa kwanza na wa ufunguzi wa michuano hii mipya unafanyika kwenye ardhi ya Tanzania.

Lakini pia michuano hii ikiwa imeanzishwa kwa mara ya kwanza inashuhudia klabu ya Tanzania kuwa miongoni mwa timu nane pekee zilizochaguliwa kwa sifa zake kushiriki michuano hii.

Simba inakuwa timu pekee kutoka ukanda wa kisoka wa Afrika Mashariki na Kati (Cecafa) kushiriki michuano hii ikiuwakilisha ukanda wote.

Hakuna ubishi kuwa haya ni mafanikio makubwa kwa Simba kama klabu lakini pia ni mafanikio kwa nchi katika upande wa soka, na ni mafanikio pia kwa Shirikisho letu la Soka Tanzania (TFF).

Lakini pamoja na juhudi za Simba zilizowapa nafasi hii ya kushiriki AFL, bado ina deni kwa watanzania kuelekea kuanza kwa mashindano haya makubwa.

Pamoja na kuwa wamepata nafasi hiyo, bado mashabiki wengi wa soka hususani mashabiki wa klabu yao, viongozi wa Shirikisho na nchi kwa ujumla wanatarajia makubwa kutoka kwao.

Simba wasibweteke kwa nafasi hii ya kuiwakilisha Cecafa kwenye michuano ya AFL, bado wana deni la kudhihirisha ubora wao kwa kufanya vizuri katika michuano hii.

Kitu kizuri michuano hii itaendeshwa kwa mtindo wa mtoano, kila timu itakuwa na mechi mbili zitakazotoa majibu ya timu gani inasonge mbele hatua inayofuata.

Tunatarajia Simba watachanga karata zao vizuri na watajiandaa vyema kufuzu hatua inayofuata bila kuangalia ni mpinzani gani watacheza naye.

Ipo wazi Al Ahly ni timu kubwa Afrika, ni Mabingwa wa Ligi ya Mabingwa, lakini pi inaongoza kwa kutwaa ubingwa huo mara nyingi zaidi kulinganisha na klabu yoyote ile.

Hata hivyo hiyo sio sababu ya Simba kushindwa kufanya vizuri, inaweza kama itajipanga vizuri na kujiandaa vyema kukabiliana nao mabingwa hao wa Afrika.

Ikumbukwe Simba imekutana mara nyingi katika miaka ya hivi karibuni na mabingwa hao wa Misri, tumeshuhudia ushindani mkubwa kwenye mechi mbili za mwisho walizokutana.

Simba ilianza kwa kushinda bao 1-0 hapa nyumbani kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku ikicheza soka safi na kuwashangaza waarabu hao.

Hata walipoenda kurudiana Misri, pamoja na kufungwa bao 1-0, waarabu hao hawakuamini na upinzani walioupata kwenye mchezo huo ambao Simba walicheza kama wapo nyumbani.

Mfano huo tumeutoa tukilenga kuweka wazi kuwa hakuna kinachoshindikana kama Simba watajiandaa vizuri na kumsoma vyema mshindani wao wanaweza kuwatupa nje na kutinga hatua inayofuata.

Lakini pia mchezo huu unafaida kubwa kwa Yanga, watani wa Simba ambao wamepangwa kundi moja na Al Ahly kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga wanaweza kuutumia mchezo huu kuwasoma Al Ahly wakiwa wanacheza na Simba na kujua namna gani watakabiliana nao kwenye mchezo wao wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Mabao 8 tu vichwa kati ya 89 Ligi Kuu, hii si ishara nzuri

**LIGI** Kuu Tanzania Bara ina mabao manane tu ya vichwa kati ya mabao 89 yaliyofungwa mpaka kufikia raundi ya tano.

Kwa michezo 40 iliyochezwa inaonekana kuna udhaifu mkubwa kwa wachezaji wanaocheza Ligi Kuu nchini iwe wa kizawa au wa kigeni kufunga kwa staili hiyo.

Jinsi mpira wa miguu unavyochezwa mara nyingi mabao hupatikana kwa njia mbalimbali, angalau kwa uchache kungekuwa na mabao 20 hivi yaliyofungwa kwa vichwa.

Halafu cha kushangaza hapa ni kwamba kati ya mabao hayo manane, pamoja na uchache wake ni moja tu limefungwa na mchezaji wa kigeni.

Fabrice Ngoma wa Simba raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, ndiye mchezaji pekee wa kigeni aliyefunga bao kwa kichwa, akifanya hivyo kwenye mchezo ambao timu yake ilicheza dhidi ya Mtibwa Sugar, Uwanja wa Manungu Complex, ikishinda mabao 4-2.

Waliobaki wote wa Wabongo, ambao ni Elias Maguri wa Geita Gold, Feisal Salum na Idd Selemani 'Nado' wote wa Azam FC, Edward Songo wa JKT Tanzania, Juma Shemvuni wa KMC, Lenny Kissu wa Ihefu bao ambalo alilifunga dhidi ya Yanga timu yake ikishinda mabao 2-1, na Paul Biswita wa Namungo.

Hapa inaonyesha pamoja na kwamba ni idadi ndogo ya mabao kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, lakini angalau hata Watanzania wameonyesha uwezo.

Kwa vyovyote vile kuna tatizo mahala, kwa wenzetu hasa ligi zilizoendelea iwe Ulaya, au Afrika hasa Afrika Kaskazini 'kwa Waarabu', kichwa ni kiungo ambacho kinaweza kukupa bao kwa urahisi zaidi kuliko mguu.

Wenzetu wanafunga sana mabao ya vichwa na ni hatari zaidi kwenye maeneo hayo kwani wanapenda sana kutumia faulo na krosi.

Ligi ya Tanzania inatajwa kuwa ni moja kati ya ligi bora barani Afrika, hivyo kuwa na mabao manane tu ya vichwa mpaka sasa inaonyesha kuwa inawezekana haipati wachezaji bora zaidi kutoka nje ya nchi, na pia mafunzo kwa wachezaji kutoka kwa makocha wao yana walakini katika matumizi ya vichwa kwenye eneo la hatari, au pia wachezaji wenyewe wana matatizo.

Kuna baadhi ya wachezaji wanapiga vichwa wakiwa wamefumba macho, hawa ni rahisi sana kukosa bao hata yeye na nyavu.

Nadhani hawa ndiyo tunao kwa kiasi kikubwa kwenye ligi yetu, kwa kawaida mchezaji yoyote hatari kwa kufunga mabao ya vichwa ni yule ambaye anapiga kichwa akiwa hajafumba macho ili aweze kuuelekeza mpira kule anakotaka uelekee.

Mchezaji wa aina hii huwa ni hatari sana kwani muda wowote anaweza akawadhuru.

Miaka ya nyuma nchi hii ilikuwa na wachezaji ambao walikuwa wakifunga zaidi mabao ya vichwa kuliko hata miguu.

Akifunga mabao sita, basi manne atakuwa ameyafunga kwa kichwa na mawili kwa mguu.

Wachezaji wa aina hii waliongozwa na Abeid Mziba wa Yanga, Jumanne Hassan 'Masimenti', aliyeichezea Cosmopolitan na baadaye Simba, Athumani Machupa na Mohamed 'Bob' Chopa, wote hawa wa Simba, Peter Tino wa African Sports, Pan African na Yanga na wengineo wengi.

Hii tayari ni kengele ya hatari si kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara tu, bali hata kwa makocha wanaofundisha timu za vijana.

Wawatengeze wachezaji ambao hawatouogopa mpira kwa kuupiga kichwa kwa ajili ya kuwaandaa na michuano ya AFCON 2027 inayotarajiwa kufanyika hapa nchini, Kenya na Uganda ambapo Stars moja kwa moja itacheza fainali hizo.

Kwa wachezaji wanaoendelea kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara wanatakiwa wabadilike kwani kama atatokea mchezaji yeyote sasa mwenye uwezo wa kwenda juu hewani kuzifuata krosi, kona na faulo, anaweza kufunga mabao mengi zaidi kwani hii ndiyo njia nzuri zaidi ya kupata mabao kwa urahisi sana kwenye mchezo wa soka.

Ugumu wake upo kwenye kujituma, kujitolea, kutokuwa mwoga wa kwenda kuushambulia mpira kwa kuupiga ukiwa juu na kuuelekeza langoni.

# TANROADS yajipanga kukabiliana na Eli-Nino

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Dar es Salaam umesema unaendelea kusafisha eneo lote la Mto Msimbazi ili kuchukua hatua za mapema kukabiliana na athari zinazoweza kutokea wakati wa mvua za El-Nino.

Kaimu Meneja wa TANROAD Mkoa wa Dar es Salaam, Mhandisi Elisony Mweladzi, aliyasema hayo na kueleza kuwa, wataendelea kufanya usafi huo ili wakati wa mvua maji yaweze kupita bila kikwazo. "Usafishwaji hautakomea kwa eneo hili la Jangwani kwenda daraja la Salender bali tunasafisha madaraja yote ili mvua zitakaponyesha kusiwe na usumbufu wowote.

"Usafishaji wa mahususi ambao ulipangwa kufanyika, ulikuwa wa kilomita mbili kutoka eneo la Jangwani mpaka daraja la Salender ambapo mpaka hivi sasa, ni mita 800 tu ndizo ambazo zimeshafanyiwa kazi ya kusafishwa," alisema.

Usafishaji huo ni maagizo ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye aliagiza mikoa kumi ambayo itaathirika wakati wa mvua hizo zikianza kuhakikisha miundombinu yote ya maji pamoja na maeneo hatarishi yanafanyiwa matengenezo ili kuepuka madhara makubwa.

Msimamizi wa Mradi huo kutoka Kampuni ya BECCO, Enhard Sebastian, alisema wapo tayari kumalizia eneo lililobaki. Mkazi wa Tabata, Shelemia Gwassy, ameishukuru serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuamua kusafisha mito na kuomba kuwapo kwa utaratibu mzuri wa uzoaji taka katika makazi ya wananchi.

# Ubalozi wa Sweden waandaa matembezi tahadhari saratani

**Na Beatrice Shayo**

UBALOZI wa Sweden kwa kushirikiana na Shujaa Cancer Foundation umeandaa matembezi ya hisani kupambana na ugonjwa wa saratani yanayolenga kutoa tahadhari kuhusu pengo la huduma ya saratani.

Balozi wa Sweden nchini, Charlotta Macias, aliyasema hayo jana Dar es Salaam kwamba matembezi hayo yatafanyika Oktoba 21, mwaka huu, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, kampuni ya kiswidi, Taasisi ya Kansa ya Ocean Road na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Alisema saratani ya matiti ni ya kawaida zaidi kwa wanawake ulimwenguni na makadirio ya hivi karibuni ya wagonjwa wapya milioni 2.1 kwa mwaka.

"Saratani ya matiti ndiyo chanzo kikuu cha vifo vinavyohusiana na saratani miongoni mwa wanawake duniani kote, huku zaidi ya vifo 600,000 vinaripotiwa kila mwaka na asilimia 62 kati yake, hutokea katika nchi zinazoendelea," alisema.

Balozi huyo alisema saratani ya matiti nchini Tanzania imeripotiwa kwa kiwango kidogo katika miongo miwili iliyopita.

Alisema takribani asilimia 80 ya wagonjwa wa saratani ya matiti hugunduliwa katika hatua ya mwisho kutokana na upatikanaji mdogo wa program za uchunguzi, utambuzi wa awali, upatikanaji duni wa matibabu kama vile tiba kemia, upasuaji na tiba ya mionzi.

Alisema uchunguzi umeonyesha kuwa asilimia 6.5 ya wagonjwa wote wa saratani ya aina hiyo ni wanaume ambayo ni zaidi ya mara 10 ya idadi inayoonekana katika sehemu nyingi duniani.

Pia alisema lengo la matembezi hayo ni kukuza uelewa kuhusu umuhimu wa kupima saratani ya matiti na kujipima.

"Tunalenga kusaidia wale walioathiriwa na saratani ya matiti na kuangazia umuhimu wa utafiti, kuzuia, matibabu na kupona kutokana na madhara ya matibabu na kuongeza ufahamu wa saratani ya matiti kwa wanaume na wavulana,"alisema Balozi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shujaa Cancer Foundation, Gloria Kida, alisema kampeni ya wiki ya uhamasishaji wa uelewa wa saratani ya matiti mwaka huu inakwenda sambamba na mkakati wa Wizara ya Afya wa kukabiliana na saratani na kupunguza athari kwa jamii na kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa uchunguzi na matibabu mapema.

Alisema saratani ya matiti si ugonjwa wa wanawake pekee wapo wanaume wanaoshikwa na maradhi hayo jambo la msingi ni kujifanyia uchunguzi na ukibainika una shida upatiwe matibabu kwa wakati.



Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Kheri James (katikati) akiwa na mwenge wa uhuru baada ya kiongozi wa mbio za mwenge wa uhuru, Abdalah Shaibu Kaim (watatu kulia) kuzindua mradi wa maji Kijiji cha Qalieda juzi, watatu kushoto ni Meneja wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoani Manyara, Mhandisi, Walter Kirita. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mkuu wa Mkoa ataka mbinu zaidi matumizi ya bima

**Na Restuta James**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ametaka mbinu na elimu zaidi kwa wananchi ili wakubali kutumia huduma za bima kwa hiari.

Aliyasema hayo jana Dar es Salaam, katika semina ya mawakala wa bima iliyoandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania (TIRA) kwa kushirikiana na Shirika la Bima la Taifa (NIC)

Chalamila alisema wadau waliopo kwenye sekta hiyo wana kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha Watanzania wengi wananufaika na bima ifikapo 2030.

"Nawapa changamoto mje na ubunifu utakaowafanya watu wakate bima bila shuruti, watu waache kukata bima kwa ajili ya kumkwepa askari barabarani, bali wafurahie kupata huduma hii muhimu," alisema.

Chalamila alisema njia ya kuwafikia wananchi wengi ni kuongeza kasi ya kutoa elimu na kubuni bidhaa zitakazowavutia watu kuzitumia.

Alisema kampuni za bima pamoja na mawakala wake zinapaswa kutumia fursa ya kufunguka kwa nchi kiuchumi na kiuwekezaji, kwa kufanyakazi kwa uaminifu ili wawekezaji wafurahie huduma za bima nchini.

Alisema kuna uwekezaji unaendelea kwenye ujenzi wa viwanda pamoja na shughuli nyingine za biashara ambazo zinahitaji huduma za bima.

Chalamila aliwataka wakazi wa Dar es Salaam na Watanzania kwa ujumla kukata bima ya mali, maisha na matibabu ili wawe salama pindi wanapokutwa na majanga.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa NIC, Mkurugenzi wa Bima za Maisha wa shirika hilo, Hudbert Polepole, alisema wataendelea kutoa elimu kwa umma ili watu wengi zaidi wawe salama pindi wanapopata matatizo. "Ni muhimu wananchi wafahamu kuwa, ukiwa na bima hakuna mali yako yoyote itakayoathirika. Sisi tutaendelea kubuni bidhaa bora na kutoa elimu kwa umma. NIC ina soko na mtandao mkubwa wa mawakala nchi nzima ambao wanaweza kutoa huduma kwa watu wengi ndani ya muda mfupi," alisema.

Meneja Ukaguzi wa TIRA, Frank Shangali, alisema sekta ya bima ina aina tisa ya watoa huduma zikiwamo bima mtawanyo, madalali, mawakala, wathamini wa majanga, uchunguzi, benki na digitali.

Alizitaka kampuni na mawakala wa bima, kuhakikisha hayatumiki kutakatisha fedha haramu kupitia sekta hiyo.

Pia alisema watafanyakazi na wadau wote kulinda watoa huduma na wateja, ili kuhakikisha kila upande unapata haki stahiki.

Awali, Mwenyekiti wa Chama cha Mawakala wa Bima Tanzania (IAAT), Sayi Daud, alisema kuna mawakala 1,300 wa bima nchini ambao wanawajibu wa kutoa elimu kwa umma.

Aliomba serikali iondoe kodi ya mabango ya bima ili mawakala waendelee kutoa elimu pamoja na kodi ya huduma kwa mawakala na badala yake ibakie kwa makampuni ya bima.

# Chongolo awakumbusha wajibu viongozi

**Na Neema Hussein,**
SUMBAWANGA

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amewataka viongozi wa serikali kunawahudumia wananchi na kutatua changamoto zao ili kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kuyafikia malengo yaliyokusudiwa.

Chongolo aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa mkoa wa Rukwa wakati akihitimisha ziara yake ya siku nne mkoani hapa.

Alisema, katika maeneo waliyotembelea, kuna miradi ambayo imekamilika lakini kuna maeneo ambayo haijakamilika hivyo, kutoa maelekezo kwa viongozi kuhakikisha inakamilika kwa haraka.

Miradi hiyo, alisema ni pamoja na ya maji ambayo alielekezwa kwamba ile ambayo haijakamilika itekelezwe haraka ili kuwaondolea wananchi adha ya kupata huduma hiyo.

Kuhusu elimu, alisema ni kazi kubwa ya mabilioni ya fedha yaliyoshushwa kwa kipindi kifupi na shule zimejengwa kwenye kila kata na watoto wanasoma

Pia alisema mkoa wa Rukwa ulikuwa na tatizo la umeme lakini sasa limepungua kwa kiwango kikubwa baada ya serikali kupeleka umeme na vijiji vilivyobaki ni chini ya 30, hivyo akaelekeza mpaka Desemba 30, mwaka huu, vijiji vyote vipate nishati hiyo.

Chongolo alisema maelekezo ya Raisi ni kuhakikisha nguzo za umeme zinaongezwa kutoka 20 kila kijiji hadi 60 ili kulala na vibatali iwe hadithi kwa wananchi.

"Kazi mnafanya kikubwa ni wajibu wa serikali kuleta miradi ili mneemeke na shughuli mnazofanya. Kuna suala la mahindi wako watu wawajalipwa. Tunaiagiza Wizara ya Kilimo kuwalipa haraka ili watu waendelee na msimu ujao wa kilimo.

"Tunaiagiza Wizara ya Kilimo mahindi yaliyokwa wananchi yananunuliwa na mbolea mwaka huu waisogeze kwa wananchi siyo iishie wilayani," alisisitiza.



Naibu Meya wa Jiji la Tanga, Rehema Kasimu (wa pili kushoto) akimpatia cheti Mwalimu wa Shule ya Msingi Usagara, Faraja Mwajike kwa kutambua mchango wake katika suala la Usalama Barabarani. Kushoto ni Meneja wa Amend Tanzania, Simon Kalolo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanufaika SDF waipa neno serikali

**Na Joseph Mwendapole**

WANUFAKA wa Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF), wameishauri serikali kuongeza fedha kwenye mfuko huo ili vijana wengi wanufaike na mafunzo yatakayowasaidia kujiajiri.

SDF inasimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na tangu kuanzishwa kwake mwaka 2017, imeshawanufaisha vijana 49,000.

Walitoa ushauri huo juzi ana wakati wa maonyesho ya Wiki ya Elimu ya Watu Wazima, yanayoendelea kwenye viwanja vya stendi ya zamani Kibaha mjini.

Mmoja wa wanufaika hao, Esther Shebe, ambaye ni mjasiriamali wa uyoga, alisema alipata elimu ya kilimo cha zao hilo na kusindika bidhaa mbalimbali baada ya kupata mafunzo kupitia mfuko huo.

Alisema SDF ndiyo iliyomwezesha kupata mafunzo kwenye Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) na amemudu kutengeneza bidhaa mbalimbali ambazo zinamwezesha kujikimu kimaisha.

Kazi zake, alisema zimemwezesha kupata tuzo mbalimbali na mwaka 2022 alipata tuzo ya Malkia wa Nguvu upande wa kilimo biashara ambayo huendeshwa na moja ya vituo vya televisheni nchini.

"Nashukuru SDF na TEA kwa mafunzo haya na yamenifanya nijitegemee kwa hiyo mfuko huu uwezeshwe fedha nyingi ili vijana wengine wapate mafunzo na kujiajiri badala ya kumaliza shule na kuanza kuhangaika kutafuta ajira.

"Namshukuru pia Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuona kwamba kupitia mfuko huu wanawake tunaweza kupata fursa mbalimbali kwa hiyo kitu cha muhimu ni kuhakikisha SDF inakuwa endelevu," alisema Shebe.

Mnufaika mwingine, Juma Munyi, alisema kupitia mfuko huo amepata mafunzo kupitia SIDO mkoa wa Mbeya na kuanza kuzalisha viungo mbalimbali vya chakula.

Alisema amefanikiwa kuwa mahiri kwenye kutengeneza viungo mbalimbali vya chakula na kuingiza kipato ambacho kimemwezesha kuajiri wahitimu wawili wa vyuo vikuu na amekuwa akiajiri watu wa muda wanaofikia 10 hadi 15.

"Mimi nilihitimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) mwaka 2019. Baada ya hapo niliajiriwa sehemu nikafanya kazi mwezi mmoja na nusu nikaacha baada ya kuona maslahi ni madogo, nikapata hii fursa nikaenda SIDO nikajifunza utengenezaji wa viungo," alisema Munyi.

Alisema vijana wengi wanaomaliza vyuo vikuu wanapata shida kupata ajira hivyo kuna umuhimu serikali ikaongeza fedha kwenye mfuko huo ili vijana wengi wapate mafunzo yatakayowawezesha kujiajiri na kuajiri wenzao.

"Changamoto ya ajira ni kubwa na hapa nilipofika mimi kuna vijana wengi ambao wangependa wawe kama mimi kwa hiyo mfuko kama SDF ni muhimu kuwapa ujuzi wa kujiajiri vijana kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali badala ya kukaa kusubiri ajira," alisema

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TEA, Eliafile Sola, alisema SDF imekuwa ikitoa ruzuku ya mafunzo ya ujuzi kwa vijana ambayo yanalenga kuwapa ujuzi ili waweze kuzalisha bidhaa mbalimbali na hatimaye waweze kujitegemea.

Alisema, katika maonyesho hayo wamewashirikisha baadhi ya wanufaika wa mafunzo hayo ya kuendeleza ujuzi ambayo yalianza kutolewa kwenye mikoa mbalimbali mwaka 2018 na kukamilika mwaka 2023.

"Mafunzo hayo yalitolewa kwenye sekta sita za kipaumbele ambazo ni sekta ya nishati, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kilimo, usafirishaji, ujenzi, utalii na huduma za kkaribu na hapa tuko na mmoja ambaye aliamua kujikita kwenye kilimo cha uyoga na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na uyoga," alisema Sola.

Alisema mnufaika mwingine ameamua kujiajiri kwenye kuongezea thamani bidhaa mbalimbali za viungo vya mboga mboga ambapo amekuwa akinunua kwa wakulima na kuongezea thamani.

"Hawa wanufaika ambao tunao leo ni wahitimu wa vyuo vikuu na walishawahi kufanyakazi, mmoja alikuwa muuguzi serikalini akaacha ajira ya serikali akaweka nguvu kwenye ujasiriamali, huyu mwingine alikuwa mwalimu akaacha ualimu na leo hii ameajiri vijana wengine hii inaashiria kwamba haya mafunzo ni muhimu," alisema.

## Kasekenya ataka teknolojia rafiki katika mazingira

**Na Beatrice Shayo**

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, amewataka wadau wa ujenzi nchini wajikite katika ubunifu wa matumizi ya teknolojia ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Amesema sekta ya ujenzi kwa mwaka 2022 imechangia Pato la Taifa (GDP) kwa asilimia 16 na kwamba matarajio ni pato kuongezeka kwa kipindi cha mwaka 2023 na miaka ijayo.

Kasekenya aliyasema hayo juzi Dar es Salaam wakati akifungua maonyesho ya siku tatu ya ujenzi (Construction Expo 2023) yanayoshirikisha zaidi ya kampuni 120 kutoka ndani nan je ya nchi.

Alisema sekta hiyo ni muhimu na mahitaji yanakuwa, nyumba za makazi uhitaji ni milioni tatu, huku ukuaji ukiwa ni wastani wa nyumba 200,000 kila mwaka nchini.

"Tanzania hii lazima tuijenge sisi na Watanzania ni sisi. Makandarasi lazima tusimamie ubora. Makandarasi nchini kuwa na kazi bora ili miaka ijayo kazi zinazofanywa na wakandarasi kutoka nje ya nchi zihamie mikononi kwenu kwa asilimia 100," alisema.

Kasekenya alisema hivi sasa miradi mikubwa ya maendeleo kama vile Reli ya Kisasa (SGR), mradi wa mabasi ya mwendokasi na Bwawa la Mwalimu Nyerere, inatekelezwa na makandarasi wa nje kwa kiwango kikubwa, kutokana na wazawa kushindwa kupata zabuni kwa sababu tofauti.

"Sababu mojawapo ya Watanzania kushindwa kupata miradi ya ndani ni uhaba wa mitaji, vifaa na ushirikiano miongoni mwao. Iko haja ya Watanzania kufanya kazi za ndani ili fedha zinazotumika kwenye miradi zibaki nchini kwa kiwango kikubwa.

"Ubora duni wa kazi kwenye ujenzi na kutofanyika kwa muda, kumekuwa ni miongoni mwa sababu za wakandarasi wazawa kukosa zabuni za ujenzi katika miradi ya maendeleo inayoendelea nchini na hata wakiwemo ni katika kazi ndogo,"alisema.


Alisema serikali inaunga mkono kwa taasisi binafsi kuchangamkia fursa na jambo la msingi wanalotakiwa ni kuzingatia ubora wa kazi na kukamilisha kwa wakati.

Mkurugenzi na Mwandaaji wa Maonyesho hayo, Deogratius Kilawe, aliiomba serikali iwape kipaumbele wazawa katika miradi inayofanyika nchini ya masuala ya ujenzi.

Alisema, wakati mwingine wanakabiliwa na changamoto ya baadhi ya watumishi kuomba asilimia ya fedha ya utekelezaji wa mradi kutoka serikalini jambo ambalo linawaathiri.

Pia, alisema maonyesho hayo yana lengo la kuwakutanisha wadau wa sekta ya ujenzi na kujadiliana njia mbalimbali zitakazosaidia kuinua sekta hiyo na kukuza mahusiano na kujipatia wateja wa bidhaa zao.

Nipashe
JUMAMOSI OKTOBA 14, 2023



14
OKTOBA

# KUMBUKUMBU
## MIAKA 24 YA
## MW JULIUS NYERERE



# Umoja wa kitaifa bado ni nguzo ya amani Tanzania



Madaraka Nyerere,

**Na Vitus Audax,** BUTIAMA

MIAKA 24 iliyopita taifa la Tanzania na dunia kwa ujumla ilikumbwa na majonzi kwa kumpoteza aliyekuwa mpigania uhuru na haki katika nchi za Afrika na Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere.

Nyerere alifariki dunia Oktoba 14, 1999 katika Hospitali ya Mtakatifu Thomas mjini London, Uingereza, alipokuwa akipatiwa matibabu.

Mwalimu Nyerere pamoja na kwamba ni miaka 24 tangu alipoaga dunia, ameendelea kukumbukwa kwa namna tofauti ndani na nje ya Tanzania kutokana na mchango wake katika kuleta uhuru, umoja na mshikamano si kwa Tanzania pekee bali kwa nchi za Afrika ambako inaelezwa kuwa malengo yake bado hayajatimia kama ilivyokuwa ndoto yake ya muda mrefu.

(Godfrey) Madaraka Nyerere, ni mtoto wa sita kati ya watoto wanane wa Nyerere ambaye pia ni msimamizi wa Makumbusho ya Baba wa Taifa yaliyoko katika kijiji cha Mwitongo, Butiama mkoani Mara, anasema maono ya Baba wa Taifa bado hayajafikiwa juu ya kuiunganisha Afrika kuwa moja.

"Kumuenzi Baba wa Taifa lazima tukumbuke yaliyokuwa maono yake ikiwa ni pamoja na kuifanya Afrika taifa moja na yenye serikali moja inayojitegemea katika kila kitu. Nina Imani kuwa angekuwepo mpaka sasa lazima angekuwa anasisitiza juu ya hili," alisema Madaraka wakati akizungumza katika mahojiano maalumu na mwandihi wa makala hii.

Madaraka alisema kuondoka katika familia hiyo na taifa kwa ujumla bado yako mengi ya kukumbuka na kuyafanyia kazi lengo likiwa ni kuiona Tanzania na Afrika iliyo bora kimaendeleo katika uchumi, siasa, miundombinu na utalii.

"Mambo ambayo angekuwa bado anayafikiria kichwani kwake mpaka leo ni pamoja na kuhakikisha tuna umoja wa kitaifa ikiwa ni ngazi ya kuhakikisha kuwa kuna umoja wa bara la Afrika, kutimiza malengo ya nchi huru za Afrika yaliyowekwa mwaka 1963 ambayo mpaka sasa hayajatimizwa," alisema.

**UMOJA WA KITAIFA**

Kuhusu umoja wa kitaifa, Madaraka alisema Tanzania bado ipo nafasi ya kuhakikisha maendeleo yanafanyika bila ya kuvuruga umoja, amani na mshikamano aliouacha Mwalimu Nyerere.

Alitaja suala pekee linaloweza kuligawanya taifa kuwa ni siasa kwa kuwa wako wanaoifanya siasa kuwa sehemu ya kujinufaisha, hivyo kutoa wito kwa wanasiasa nchini kumuenzi Baba wa Taifa kwa kudumisha amani na umoja bila kujali itikadi zao za kisiasa.

Licha ya kujipambanua kama si muumini wa siasa, Madaraka alitaja hali ya siasa ya Tanzania kuwa ya mvutano zaidi kuliko kushauriana na kupeana mawazo ya kujenga na kuinua uchumi wa taifa na watanzania kwa ujumla, hivyo kuwataka wanasiasa kuitumia vyema fursa ya siasa huru iliyopo kwa sasa.

"Nitoe tu wito kwa Watanzania wote kuwa katika tofauti zao za kisiasa na misimamo tofauti tofauti walinde umoja wetu. Nimnukuu tu Mwalimu Nyerere aliposema 'Tupingane lakini tusipigane.' Tuelekeze hoja zetu katika kuimarisha amani aliyotuachia Baba wa Taifa," alisisitiza.

**PENGO KWA FAMILIA**

Madaraka alisema Mwalimu Nyerere katika familia alikuwa nguzo na msingi wa maendeleo. Yeye hakupenda kuunganisha masuala ya siasa kwa maana ya utawala pamoja na familia, hivyo kuijenga familia yake katika kujitegemea.

Alisema katika mapumziko yake, alipenda kuona watoto wanashughulika zaidi katika masuala ya kilimo pamoja na ufugaji kama ilivyokuwa utamaduni wao ili kuhakikisha wanajijengea uchumi binafsi.

Alisema Mwalimu mwenyewe alikuwa mfano pale alipokuwa nyumbani hakupenda kutumia muda mwingi kupumzika bali alihitaji kushughulika na masuala ya shambani ambako ilifikia wakati wageni wanafika kumtembelea na kufikia shambani ambako pia aliweka jembe la ziada kwa ajili ya mgeni yeyote aliyefika nyumbani hapo.

"Hapa hakupenda ufike uanze kuzungumza naye tu wakati akiwa kazini bali ilibidi uendelee na kazi aliyokuwa akiifanya wakati mnaendelea na mazungumzo. Hili lilitufundisha kuwa sehemu kubwa ya maisha yetu lazima tuwekeze katika kufanya kazi," alisimulia

Katika kuthibitisha hilo, nyumbani kwa Mwalimu, Mwitongo, kuna maghala mbalimbali aliyotumia kiongozi huyo kutunzia chakula kilichovunwa shambani huku kukiwa na ulezi ambao unaelezwa kuwa ulivunwa mwaka 1998 kabla ya kuugua.

"Kwa sasa siku hii tunaipokea kawaida kama ilivyo kwa Watanzania wengine ni tofauti na siku zile za mwanzo ambazo tulikuwa tukijikuta katika majonzi makubwa na kuifanya siku ya maombolezo.

Kwa sasa tunafanya kuenzi aliyoyatenda na kumwombea pia," alisema.




# KUMBUKIZI YA MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE

**Na Mwandishi wetu**
Wakati Tunamkumbuka Mwalimu Nyerere, Umoja wa Mataifa waipigia mfano Tanzania

"Kinara wa Mfano wa kuwajibika Miradi ya Maji ya Matokeo"

"Inawezekana, timiza wajibu wako" ni moja ya nukuu za Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakati wa maisha yake. Leo Oktoba 14 tunamkumbuka kiongozi huyu aliyeongoza nchi yetu na kuhakikisha maendeleo yanamfikia kila Mtanzania, mjini na vijijini.

Ikumbukwe mwaka 2022 ilikuwa ni miaka 100 tangu kuzaliwa kwa kiongozi huyu mahiri kabisa barani Afrika.
Wizara ya Maji katika kuwaletea wananchi maendeleo , pamoja na viongozi wake inatimiza wajibu kwa kuhakikisha mjini na vijijini wananchi wananufaika na huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza.

Kazi mbalimbali zinaendelea katika kila kona ya nchi yetu kufikia lengo la upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa asilimia 85 vijijini na mijini 95. Kwa mapinduzi yanayofanyika katika miradi ya Sekta ya Maji hadi mwezi Desemba 2022 hali ya upatikanaji wa huduma ya maji hapa nchini ilikuwa asilimia 88 mijini na vijijini asilimia 77.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiongea na mwandishi wa makala hii hivi karibuni amesema Wizara anayoiongoza inatekeleza programu ya uendelevu wa huduma ya Maji na usafi wa Mazingira Vijijini kwa kutumia utaratibu wa malipo kwa matokeo (Program for Results – PforR), sanjari na nchi nyingine zaidi ya 40 Dunia kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB.)

Mhe. Aweso ameweka bayana kuwa kutokana na ushirikishwaji wa wananchi na uwajibikaji kumeleta matokeo bora, Sekta ya Maji awali ilipata dola 350 million na ndani ya miaka mitatu ilikuwa imepeleka maji kwa zaidi ya wanufaika wapya maeneo ya vijijini milioni 4.7.

Amesema kazi hiyo imewezesha wananchi milioni 6.6 kuwa na vyoo bora vijijini katika Mikoa 17 ikiwa ni matokeo makubwa kuliko nchi nyingine Duniani zinazotekeleza miradi kwa Mpango wa Matokeo chini ya Benki ya Dunia (WB).


"Kwa ufanisi huo mkubwa na mapinduzi katika Sekta ya Maji kwa nchi ya Tanzania WB imeongeza fedha kwa Tanzania kiasi cha Dola milioni 300 na sasa programu hiyo inatekelezwa katika mikoa 25 ikiwemo minane ambayo awali haikuwemo" Mhe. Aweso ameweka hayo bayana kuwa kazi ya kutimiza wajibu na kuwashirikisha wananchi kumeleta furaha zaidi kwa jamii.

Anasema ni jambo la msingi kabisa kwa viongozi katika ngazi mbalimbali kuipa ushirikiano thabiti Sekta ya Maji katika kuendeleza kazi nzuri kwenye programu hii ikiwa ni pamoja na kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maji ambapo tayari shillingi milioni 970 zimekwishapelekwa kwa kila halmamashauri zikiwa jumla ya 52 kwenye mikoa ambayo ilikua hainufaiki hapo awali.

Kupitia programu ya Lipa kwa Matokeo (PforR) Wizara ya Maji imetekeleza zaidi ya Miradi ya Maji 1,500 ambayo imekamilika na inatoa huduma kwa wananchi.

Aidha, pamoja na mafanikio hayo, kazi inaendelea ambapo mapema mwezi Machi 2023 Mhe. Aweso (Mb) alimwakilisha Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kikao cha Umoja wa Mataifa (UN) kinachohusu maji Machi 2023.

Ni mkutano wa UN uliofanyika baada ya ule uliofanyika miaka ya 70 ambapo Mhe. Aweso Pamoja na kushiriki, alihutubia mkutano kuitaka Dunia kuona umuhimu wa kusimamia agenda ya maji, thamani ya maji katika maisha na uchumi na kuongeza uwekezaji katika sekta ya maji, ushirikiano wa kimataifa katika suala la maji na kutafuta fedha kwa ajili ya maji.



**Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akimwakilisha Rais Mhe. Samia katika mkutano wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu maji, uliofanyika mwaka huu 2023, New York.**

Tanzania ilibeba agenda mbili mahsusi katika mkutano huo, utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Tatu yenye thamani takriban Dola za Marekani bilioni 6. 47 kwa kipindi cha 2022-2025.

"Nimeshiriki kikao kilichoratibiwa na Benki ya Dunia (WB) jijini New York Marekani kinachohusu Maji na Mazingira kilichohusisha Mawaziri wa Maji wa nchi mbalimbali ikiwa ni pamoja mijadala ya viongozi hao, (Ministerial Roundtable) pamoia na wadau wa maji ikiwa ni muendelezo wa vikao vya juu vya Mawaziri wa Maji kwa ajili kuongeza msukumo na mabadiliko katika kufikia dhima ya watu kupata maji safi, salama na ya kutosheleza katika Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika." Mhe. Aweso amesema.

Anaongeza kuwa alizungumzia na kuweka mkazo katika mkutano huo umuhimu wa Dunia kukaa pamoja na kusimamia ajenda ya maji; thamani ya maji katika maisha na uchumi; kuongeza uwekezaji katika eneo la maji; ushirikiano wa kimataifa katika maji; pamoja na utafutaji wa fedha kwa ajili ya maji.

Anasema baada ya kuwasilisha hotuba ya Tanzania katika mkutano huo, alishiriki katika mjadala wa Uongozi na Usimamizi wa Masuala ya Maji, ambao uliandaliwa na nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania na Afrika Kusini pamoja na mashirika mbalimbali ikiwemo Asasi inayohusika na Sekta ya Maji Duniani (GWP), Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto na Wanawake katika mataifa yanayoendelea (UNICEF) na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP).

Rais mstaafu wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Kikwete ambaye pia ni Mwenyekiti wa Asasi inayohusika na masuala ya maji Duniani (GWPSA), na Mwenyekiti mwenza wa Jopo la viongozi maarufu kuhusu Uwekezaji katika Sekta ya Maji ndiye aliyekuwa mgeni rasmi.

"Katika mchango wangu, nilibainisha Uongozi imara wa Dkt.Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano waTanzania katika agenda ya kuongeza msukumo na utashi wa kisiasa, kuongeza bajeti ya maji; na kuimarisha taasisi zinazohusiana na usimamizi wa huduma za maji na utekelezaji wa miradi ya maji." Mhe. Aweso anaweka bayana.

Aidha, aliainisha pia namna ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan ameibeba agenda ya maji kwa kutambua kuwa kupitia upatikanaji wa maji safi na salama, kuleta msukumo kwa kumuinua mtoto wa kike na mwanamke ili waweze kutumia muda zaidi katika elimu na shughuli za kiuchumi hivyo kufanikisha ajenda ya Rais ya Samia" kumtua mama ndoo kichwani " na kufikia usawa wa kijinsia katika maendeleo.

Programu ya Malipo kwa Matokeo (PforR) ni mpango ulianzishwa na Benki ya Dunia (WB) na ulianza Julai 15, 2019 ikiwa ni sehemu ya programu ya uhakika wa usalama wa maji na usafi wa mazingira vijijini.

Malengo ya PforR ni kuchochea kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Uboreshaji Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kupitia motisha zilizowekwa kwa viashiria ambavyo hupimwa kupitia mafanikio ya utekelezaji wa kazi.

Hapa Tanzania PforR imeonesha matokeo chanya na nchi Pamoja na wageni wanje lukuki wanafika kujifunza kutoka uzoefu wa Tanzania katika kufikisha huduma hii ya maji kwa jamii kwa kutambua kuwa jamii bado ina uhitaji na idadi ya watu inaongezenga.

Ni hivi karibuni wakati wa ziara katika mikoa ya kusini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mmoja wa mwananchi aliyejitambulisha kwa jina Haji Badri kutoka Mangaka alisema Wizara ya Maji inaongozwa na watafuta maji, wakiongozwa na Waziri Jumaa Aweso (Mb). Alisema, mji anaotoka wa Mangaka ulikuwa na adha kubwa ya maji, ila hivi sasa makali yamepungua na matarajio ni makubwa zaidi kwa kazi zinazoonekana kufanywa kuhusu maji. "Tusizoee changamoto na shida za wananchi" Waziri Aweso kila wakati anasisitiza jambo hili kwa watendaji wa Sekta ya Maji na wataalamu wote wa maji, hivyo jambo la msingi ni kusikiliza na kutoa majibu kwa wananchi.

Mwalimu Nyerere aliwahi kusema "hatuwezi kutatua matatizo yetu kwa kujidanga kuwa hayapo" . Serikali yetu inatambua uhitaji mkubwa wa huduma ya maji kwa wananchi na inafanya kazi saa 24 ili maji yawe msukumo wa maendeleo kwa sekta nyingine.



**Moja ya mradi wa maji kupitia Programu ya Malipo kwa Matokeo (PforR) unaotumia nishati ya jua kutoa huduma toshelevu ya majisafi kwa wananchi, Karagwe mkoani Kagera.**



# Neema Butiama katika kipindi cha miaka 24

**Na Vitus Audax, BUTIAMA**

UKIZUNGUMZIA Butiama ina maana ni eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 2,257.127 na kati ya hizo, kilometa za mraba 103 zimefunikwa na Ziwa Victoria. Butiama ambayo kwa sasa ni wilaya, ina tarafa mbili, kata 18, vijiji 59 na vitongoji 370.

Kwa muda mrefu Butiama ilikuwa chini ya wilaya ya Musoma kabla ya kuanzishwa kuwa wilaya Agosti, 2013. Kabla ya hapo ilikuwa nyuma kimaendeleo katika seklta mbalimbali zikiwamo miundombinu ya barabara, maji na umeme.

Akizungumzia mabadiliko ya Butiama kwa miaka 24 iliyopita hadi sasa, Mkuu wa Wilaya ya Butiama, Mwalimu Moses Kaegele, alisema tofauti ni kubwa kutokana na maendeleo makubwa katika sekta mbalimbali yaliyofanywa na serikali ikiwa ni sehemu ya kuenzi utendaji kazi uliotukuka wa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mwasisi wa taifa la Tanzania na aliyepigasnia uhuru wa nchi kutoka kwa wakoloni.



Licha ya kuimarika kwa hali ya usalama, amani na utulivu, pia alisema juhudi za wananchi kujishughulisha katika kilimo, ufugaji, biashara na uchimbaji wa madini zimechangia kuleta mageuzi ndani ya wilaya hiyo.

Alisema miongoni mwa vitu vikubwa vilivyofanyika katika eneo hilo ni pamoja na kuifanya kuwa wilaya mwaka 2012 kutokana na kuwako kwa mipango ya ndani ya halmashauri katika maendeleo ya sekta mbalimbali.

"Kuifanya wilaya kumesababisha mambo mengi yanakua katika eneo hili. Tukianza na suala la elimu ambako shule nyingi zimejengwa na kutokana na ongezeko la wanafunzi katika kipindi hiki cha uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan tumeongezewa shule zingine mpya nne ambazo tayari zimekamilika,"alisema Kaegele.

Alitaja barabara aliyoitumia Mwalimu Nyerere kutembea kwa mguu kwenda shuleni Musoma Mjini ambayo ililelezwa kutokujengwa kwa miaka yote na ilipoanza ilitumia zaidi ya miaka saba bila kukamilika lakini kwa sasa imekamilika kwa kiwango cha lami.

Pia alitaja vijiji vyote 59 kuwa kwa sasa vimeunganishwa na barabara hali ambayo inarahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji katika wilaya hiyo na kuwasaidia watalii kuingia na kutoka bila kukabiliana na changamoto za usafiri.

"TARURA (Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini) wameendelea kufanya kazi kubwa katika upanuzi wa mtandao wa barabara. Kwa mwaka jana tumefanikiwa kupata zaidi ya Sh. bilioni nne kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara huku fedha zingine zikiendelea kuletwa kwa mwaka huu kwa ajili

INAENDELEA UK.14

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA




*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere*

P.O.BOX 9184, Dar es Salaam, Tanzania
+255 22 2110401/5; +255 22 2110371/5; +255 22 2137631/2
Namba za Simu bure: 0800 110032, 0800110047, http://www.ports.go.tz

tanzaniaportshq
tanzaniaportshq
TPAHQ
tanzaniaportshq

*TPA The Gatway to Global Trade and Prosperty*


The Late, Former President of
The United Republic Of Tanzania
Mwl. Julius Kambarage Nyerere

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)**

# MIAKA 24 YA KUMBUKIZI YA MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE

**MIAKA 24**

**1999 — 2023**



Hayati Baba wa Taifa. Mwl. Julius Kambarage Nyerere.

Uongozi, Wanachama na Wafanyakazi wa Chama cha Walimu Tanzania, wanaungana na Mh. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania Wote kuadhimisha miaka 24 ya kumbukizi ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

CWT tutaendelea kutekeleza majukumu yetu kwa weledi ili kuchangia katika maendeleo ya nchi.

***"Mshikamano daima ndio mkombozi wetu"***

**CHAMA CHA WAALIMU TANZANIA (CWT)**
**S.L.P 3077, DODOMA**
**Barua pepe: info@ttu.or.tz**
**Tovuti: www.ttu.or.tz**



# Neema Butiama katika kipindi cha miaka 24

INATOKA UK.12



ya ujenzi na upasuaji wa barabara ambazo hazikuwapo,' alisema.

HUDUMA YA MAJI

Kuhusu hali ya upatikanaji wa maji wilayani Butiama, Mkuu wa Wilaya alisema mwaka 2013 wakati wilaya hiyo inaanzishwa, upatikanaji wa maji ulikuwa chini ya asilimia 50 licha ya idadi ya wananchi kuwa wachache kwa kipindi hicho ambako pia walikuwa wakitegemea mradi wa maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA).

Alisema hali ya upatikanaji maji imeendelea kuboreka kwa kasi kubwa ambako kwa sasa ni zaidi ya asilimia 80 na unatarajia kuongezeka maradufu pindi utakapokamilika mradi mkubwa zaidi wenye thamani ya Sh. bilioni 70.5 unaotoa maji kutoka Ziwa Victoria ambao kwa sasa umefikia asilimia 91.

Pia alisema wilaya hiyo imepokea zaidi ya Sh. bilioni 10.8 ambazo zinaendelea kutumika katika kuhakikisha miradi mbalimbali ya maji inatekelezwa wilayani humo ikiwa ni pamoja na kuchimba visima vya muda mrefu na muda mfupi kwa lengo la kuondoa kabisa adha ya upatikanaji wa maji safi na salama.

**MAENDELEO ELIMU**

Mkuu huyo wa wilaya alisema Butiama imeendelea kuboresha sekta hiyo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa shule nyingi mpya huku akitaja zile zilizojengwa kwa kipindi cha awamu ya sasa ambazo ni nne zenye thamani ya Sh. milioni 700 kwa kila shule lengo likiwa kuondoa msongamano madarasani pamoja na kuwasogezea karibu shule wanafunzi.

"Tukizungumzia kipindi hiki cha elimu bure, hapa tunaona ongezeko kubwa la wanafunzi. Serikali imejenga zaidi ya madarasa 170 yaliyojengwa na kukamilika na tayari yanaanza kutumika. Vilevile tunazo shule mpya mbili za sekondari zilizojengwa na tayari zinatumika.

Kuhusu vyuo vikuu na vya kati, Kaegele alisema kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Kilimo na Teknolojia (MJNUAT) katika iliyokuwa Shule ya Sekondari Oswald Mang'ombe kampasi ya Butiama ambacho kinaanza udahili mwaka huu, kumeleta Faraja na sura mpya ya maendeleo Butiama. Ili kufanikisha azma hiyo, alisema serikali imetoa Sh. bilioni 102 kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho.

"Kutokana na Baba wa Taifa kupenda sana kilimo, ndiyo maana serikali imeamua kuweka chuo hiki kikubwa katika wilaya ya Butiama kama sehemu ya kuenzi kazi yake iliyotukuka ya kiutumishi kwa taifa letu," alisema.

Alitaja taasisi na vyuo vingine vinavyopatikana katika wilaya hiyo kuwa ni pamoja na Taasisi ya Mafunzo ya Ufundi Stadi Kyarano, Chuo cha Biblia Kiabakari, Chuo cha Musoma Utalii na Kituo cha Mafunzo ya Kilimo Buhemba.

**UWEKEZAJI**

Kuhusu uwekezaji, mkuu huyo wa wilaya alisema kutokana na maendeleo makubwa ya wilaya hiyo wamekuwa wakifika wawekezaji na kuwekeza katika sekta ya madini huku akitaja uwapo wa migodi mitatu mikubwa na mmoja wa wachimbaji wadogo ambayo imekuwa ikiongeza kwa kasi ukuaji wa mji na wilaya hiyo.

Pia alisema wilaya hiyo imeweka mpango wa kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji zaidi, hivyo kuwakaribisha watu wote wenye nia ya kuwekeza katika wilaya hiyo kutokana na kuwa na mwingiliano mkubwa na fursa za kibiashara.

Katika kuhakikisha watumishi wanafanya shughuli zao katika mazingira rafiki na salama na kuwahudumia wananchi kwa wakati, alisema serikali inatekeleza ujenzi wa ofisi mbalimbali za watumishi wa umma, taasisi za kiserikali na halmashauri katika eneo hilo la Butiama ikiwa ni sehemu ya kuendelea kuufungua mji na wilaya kiuchumi na kiutawala.

Miaka 24 iliyopita eneo hilo la Kijiji cha Butiama halikuwa na ofisi yoyote ya kiutawala kwa kuwa huduma zote zilifuatwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma Vijijini baada ya kuanzishwa rasmi kuwa wilaya, zilijengwa chache kwa muda kwa ajili ya kutolea huduma ambazo hata hivyo hazikidhi mahitaji ya wananchi.

Kaegele alisema maendeleo katika ujenzi wa ofisi za taasisi katika kipindi kifupi ni makubwa zaidi, hivyo kuifanya wilaya kuwa sehemu yenye huduma zote muhimu na salama kwa watendaji wote.

"Wakati tunafika hapa hakukuwa na makao makuu ya halmashauri lakini kwa sasa yamejengwa kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni tatu na tayari watumishi wanaendelea na utekelezaji wa majukumu yao katika makao makuu hayo," alisema.

Katika Wilaya hiyo hakukuwa na nyumba ya mkuu wa wilaya lakini kwa sasa imejengwa. Pia nyumba ya katibu tawala imejengwa na kwamba hakukuwapo na ofisi ya mkuu wa wilaya lakini kwa sasa inaendelea kujengwa na inatarajiwa kukamilika Machi, mwakani.

Mkuu huyo wa wilaya alisema tafsiri ya ujenzi wa makao makuu ya halmashauri ni mpango wa serikali kutengeneza mazingira rafiki kwa watumishi kuendelea kutoa huduma kwa wananchi na katika mazingira rafiki.

**KUMUENZI NYERERE**

Kuhusu Halmashauri hiyo kumuenzi Baba wa Taifa, mkazo mkubwa ni kufanya kazi kwa bidii kama alivyokuwa anafanya pamoja na utunzaji wa mazingira. Kaegele alisema katika suala la mazingira, halmashauri imekuwa ikiendelea na upandaji miti kupitia matukio mbalimbali ili kuhakikisha uoto wa asili unalindwa pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Katika maadhimisho ya Kumbukumbu ya Miaka 24 ya Mwalimu Nyerere, Kaegele alisema wilaya watafanya katika makumbusho na nyumbani kwa Mwalimu Nyerere ambako alizikwa kwa kumwombea. Maadhimisho hayo kitaifa yanafanyika mkoani Manyara.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU
WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI

KUMBUKIZI YA MIAKA 24 YA KIFO CHA MWALIMU J.K. NYERERE



24 Miaka
1999 - 2023

Bodi ya Usimamizi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) wanaungana na **Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watanzania wote kuadhimisha miaka 24 ya kumbukumbu ya kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

OSHA tutaendelea kumuenzi Baba wa Taifa Hayati Mwal. Julius Kambarage Nyerere kwa kufanya kazi kwa bidii katika jukumu letu la msingi la kusimamia utekelezaji wa Sheria Na. 5 ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003.

*"Usalama na Afya Kazini Huongeza Tija"*

*Mwal. Julius Kambarage Nyerere (1922 -1999)*
*Rais wa Awamu ya Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tamzania*

TanzaniaOsha
OshaTanzania
OshaTanzania
Osha Tv Online
Simu Bila Malipo: 0800110091/2

**Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)**
P.O.Box 519, DAR ES SALAAM
Simu Na: +255 (0) 22- 27 60548
Nukushi +255 (0) 22- 27 60552
Barua Pepe: info@osha.go.tz





## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Ndivyo Nyerere alivyokuwa katika soka, sanaa na starehe yake kuu, mchezo wa bao

**Na Adam Fungamwango**

LEO ni miaka 24 hatunaye huyu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Ila tukikumbuka tulikotoka, hata akatufikisha, hatuyamalizi ya kwake.

Basi tumeamua kuwa na kiasi katika kumtafsiri, tukidadavua alikuwaje na sekta hii ya michezo na burudani.

Tuanzie hapo hapo, hivyo kwa nini wale wanajiita Klabu ya Wananchi?...Nyayo za Nyerere 'laivu', zinaonekana.

Rejea baada ya uhuru, ni namna gani watu wametumia uhuru wao kulisakata dansi vilivyo, ukichimba huku na kule, unamuona Nyerere huyooo! Au nako kuna ubishi? Jamani Msondo na Sikinde si haooo!

Hamia jeshini kidogo, unapotamka bendi ya JKT Kimbunga 'Stereo', na wadogo zao, JKT Mafunga maarufu kama Kimulimuli, huku kaka zao Mwenge Jazz ya Mashujaa, ambayo nayo baadaye ikapata mabinamu zake wengi kama CTU Les Mwenge, Mzinga Troupe na Polisi Jazz, ukiweka darubini, kupitia jembe lake kama vile mzee Moses Nnauye, pasipo kumdhulumu cheo chake cha Ubrigedia, moja kwa moja unamuona Baba wa Taifa...hapo nakuwa sijawataja walivyoibuliwa wasanii kina Kapteni John Komba.

Mwaka 1970, hakuwa na hiana kwenye maonyesho ya Expo 70 nchini Japan aligharamia sanaa ya Tanzania, ikafanya mambo mpaka leo, Mbaraka Mwinshehe Mwaruka na Morogoro Jazz, Mzee Morris Nyunyusa, ambaye ni babu yake Zuberi Katwila, mlemavu wa macho aliyekuwa na uwezo wa kupiga ngoma 10 kwa mpigo, achilia mbali simulizi za Mwalimu, maisha yake yote kutumia wasanii na wanamuziki kufanikisha maendeleo ya Tanzania.

Njoo kwenye mashirika yake ya umma, kuna burudani gani iliyokosekana kwa wale wanaoijua?

Ila kuna kitu kimoja, mpira wa Tanzania ulikuja juu kupita kiasi, hasa kuanzia miaka 10 baada ya uhuru, unajua kwa sababu gani? Hakuna na hiana, maana ni wazi alikuwa na sera yake ya 'furahieni nchi yenu.'

Hapo tena nikumegee umbeya mdogo, kwa wanaoijua ukumbi wa sinema wa Drive Inn, pale Msasani, Dar es Salaam ambako ilikuwa njia yake ya kwenda na kutoka kazini, maarufu kama Old Bagamoyo Road, eti watu wakajenga hoja ibomolewe kwa mbadala wa wanaojua wao, wakati Nyerere anajua kabisa ndiyo kijiwe cha watu wanapumzika kuangalia sinema wakiwa nje ya ukumbi huo.



Picha hii ni ya mwaka 1972 wakati Rais wa Sudan Jaffary Nimeiry akiikagua timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars'. Baada ya Stars kukosa jezi wakati wa mechi yao dhidi ya Sudan, wachezaji waliamua kuingia uwanjani wakiwa vifua wazi mpaka walipopata msaada wa jezi. Mbali na kukosa jezi, Taifa Stars pia waliingia uwanjani kwa mguu kutoka walipokuwa wameweka kambi katika Jeshi la Wokovu Mgulani baada ya kukosa usafiri. Pamoja na hayo, katika mechi hiyo Stars waliibuka na ushindi.

Aliwaka kupita kiasi na marufuku juu, hoja ikafa hapo hapo.

Watu walichojiuliza, tofauti na viongozi wengine mbona alikuwa haonekani kwenye mechi mbalimbali kubwa za klabu kubwa na timu za taifa, hasa Taifa Stars?

likatokea la kutokea uwanjani, ngumi zikatembea kwa wachezaji wa pande zote mbili, lakini hapo hapo tukashuhudia busara za kiwango cha juu cha mlindamlango Omari Mahadhi Bin Jabir, akajiweka kando kabisa na ngumi hizo, akifanya mazoezi madogo langoni mwake.

Ama kweli alikuwa ustaadhi wa uhakika.

Kwa namna walivyomheshimu Nyerere, siku ya pili simulizi hadi mashuleni ilikuwa ni kuulalamikia ugomvi huo, na ikawa mara ya mwisho kwa Nyerere kuonekana uwanjani kushuhudia soka.

Ndani ya zama hizo soka letu limenoga, mwaka 1972 ilishachezwa mechi kati ya Taifa Stars na wenzao wa Sudan kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), ikatokea hitilafu ya Taifa Stars kukosa jezi wakaona isiwe tabu, wakakubaliana na makamisaa ya mchezo, wakazama uwanjani tumbo zake na kukaguliwa na mgeni rasmi, Rais wa Sudan wakati huo, Jaffar Nimeiry.

Kule kwetu uswahilini kuna msemo tunautoa kwa kutangulia na mbwembwe za kuropoka, 'hallooo... makubwa hayo madogo yana nafuu!' Nami nikumegee, unashangaa ya tumbo wazi, lakini timu iliingia uwanjani kwa miguu kutoka ilipoweka kambi, maeneo ya Jeshi la Wokovu, kwa wasiojua ni maeneo ya Uhasibu, lakini wakasakata soka kwa kiwango cha juu, na bila shaka, wakijiamini kweli kweli na wakatoka na ushindi.



Hao ndiyo vijana wa Nyerere, uzalendo kwanza maslahi baadaye.

Mechi nyingine ilipigwa miaka kama mitatu baadaye nayo ina simulizi yake, Taifa Stars ilipambana na timu ya taifa ya Ethiopia, tukasikia mgeni rasmi ni Mwalimu Nyerere, umma wote ukaitia 'wao!', sasa mambo yamenoga, Mwalimu uwanjani.

Katika zama hizo, kiungo namba nane Sunday Manara, na mshambuliaji, Abdallah Kibaden 'King' walikuwa kwenye kiwango cha juu kabisa, Taifa Stars ni moto kweli kweli.

Lakini Mungu kamuumba kila mtu na ulevi wake, mtu anaweza kukataa kila kitu kitamu anacholetewa kwenye sherehe, ila utafiti vionjo vyake, usishangae kagomea pilau kwa nyama, na soda juu, sasa msongee ugali kwa nguru wa kuchoma na tongwa yake pembeni, hapo umemfikisha, tabasamu lake la sandukuni analiibua bila hiana.

Ndiyo namna anapopatikana Nyerere, kwa mchezo wa bao we acha tu! Waliocheza naye, wana ushuhuda akiwamo marehemu binamu yake, mzee Nyang'ombe Warioba, mwenyewe alikuwa akimtania 'huyo karogwa na bao', ingawaje ukishuhudia naye Nyang'ombe anapopambana na Nyerere kwenye dabi ya bao, unagundua naye karogwa vile vile.

Hapo ni ubishi, unachukua hadi saa sita za usiku, inafikia hatua gemu linalala linaendelea siku ya pili, mbwembwe za Nyang'ombe kwa Nyerere 'wewe hamna kitu', Mwalimu naye akimjibu kwa kumponda kwamba shule yake ni ndogo, huku majidai yake anawanunulia soda watazamaji wote waliozunguka hapo kushuhudia mechi hiyo. Nani anasema Butiama hapalipi?

Daima upenzi huo wa mchezo wa bao Mwalimu amesafiri nao muda wote hadi tarehe za mwisho yake, ikimfanya afurahie maisha ya Butiama na ustaafu. Sasa tujiulize, unasaba wa Mwalimu na burudani, michezo na sanaa upoje?

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

# Israel yatoa saa 24 kuhama Gaza

## -Waandaa jeshi, vifaru na mabomu mazito

**TEL AVIV,** ISRAEL

WAKATI mapigano makali yanaendelea Ukanda wa Gaza kwa siku nane mfululizo, jeshi la Israel limesema wamedondosha mabomu 6,000, yenye uzito wa tani 4,000, katika eneo hilo linalotawaliwa na kundi la Hamas.

Jeshi hilo limeeleza mashambulizi hayo ya anga yataongezeka maradufu hadi pale watakapohakikisha wanamgambo wa Hamas wameangamizwa.

Jana jeshi hilo lilitoa taarifa kwa Umoja wa Mataifa, ikiwataka kila mtu anayeishi kaskazini mwa Gaza aondoke haraka ndani ya saa 24 na kwenda Kusini mwa eneo hilo ili kuepuka mashambulizi ya anga.

Umoja wa Mataifa ulisema takriban watu milioni 1.1 ambao nusu ya wanaishi Ukanda wa Gaza.

Tahadhari hiyo ilitolewa kabla ya usiku wa manane wa jana.

"Umoja wa Mataifa unaona kuwa haiwezekani kwa harakati kama hiyo kufanyika bila matokeo mabaya ya kibinadamu," ulisema umoja huo.

Israel ilikuwa inajiandaa kwa mashambulizi ya ardhini, inakusanya wanajeshi, mizinga mikubwa na vifaru kwenye mpaka wa Gaza.

Imekuwa ikifanya mashambulizi ya anga mjini Gaza tangu Jumamosi baada ya wanamgambo wa Hamas kuishambulia Israel kwa kushtukiza.

Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Lloyd Austin, aliwasili jana nchini Israel siku moja baada ya ziara ya waziri wa mambo ya nje Antony Blinken.

Austin alikutana na Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu, Waziri wa Ulinzi Yoav Gallant na Baraza la Mawaziri la Vita vya Israel.

Kwa mujibu wa maofisa wa ulinzi wa Marekani walioandamana na Austin, ziara hiyo inalenga kusisitiza uungaji mkono usioyumba wa Marekani kwa Israel na dhamira yake ya kuhakikisha nchi hiyo ina kila inachohitaji kujilinda.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani Annalena Baerbock na Rais wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya Ursula von der Leyen pia wanatarajiwa kuwasili Israel.

Kwa upande wake Rais wa Brazil Luiz Inacio Lula da Silva, ambaye anashikilia urais wa zamu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, aliitaka Israel kuweka njia itakayozingatia maslahi ya kibinadamu kwa ajili ya wakazi wa Gaza kuhama kuelekea Misri.

Kupitia mtandao wa kijamii wa X, Rais Lula alisema amezungumza kwa simu na rais wa Israel Isaac Herzog na kutoa wito wa kuzingatia ubinadamu ili watu wanaotaka kuondoka Ukanda wa Gaza kupitia Misri wawe salama.

Mbali na Lula, viongozi mbali mbali wa Ulaya na Shirika la Afya Ulimwenguni wametoa wito wa kuundwa njia salama ambayo watu wanaweza kutumia kuondoka eneo la Palestina na kuruhusu misaada ya kibinadamu kuingia.

Brazil pia imeitisha mkutano wa Baraza la Usalama siku ya Ijumaa kujadili mzozo unaoendelea.

Data ya wakimbizi waliosajiliwa wa Palestina na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuwahudumia wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA) limesema limehamishia makao yake makuu kusini mwa Ukanda wa Gaza kufuatia wito wa Israel wa kuwahamishia.

Shirika hilo linawapa hifadhi zaidi ya asilimia 60 ya watu 423,000 waliokimbia makazi yao katika siku za hivi karibuni katika Ukanda wa Gaza.

Huku haya yakijiri Umoja wa Mataifa umetoa ombi la dharura la dola milioni 294 kushughulikia mahitaji ya dharura ya watu huko Gaza na Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kwa mabavu huku mapigano kati ya Israel na kundi la wanamgambo wa Hamas yakiendelea.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA) lilisema fedha hizo zitatumika kusaidia zaidi ya watu milioni 1.2.

Aidha OCHA imeeleza kwamba vituo vya matibabu pia vimejaa ikiwa ni pamoja na wanawake wajawazito 50,000 ambao sasa wanakabiliwa na matatizo ya kupata huduma muhimu za afya.

**BBC**



Wakazi wa Gaza wakiwa katika harakati ya kuhama mji huo baada ya jeshi la Israel kutoa saa 24 wawe wameondoka **PICHA:REUTERS**

## Kenya yahofia shambulio la kigaidi

**NAIROBI,** KENYA

KENYA imeonya kuwepo kwa tishio la shambulio la kigaidi lililopangwa kufanywa na kundi la Al-Shabaab.

Shambulio hilo ni kama nia ya kuonyesha mshikamano baada ya shambulizi la Hamas nchini Israel mwishoni mwa juma lililopita.

Taifa hilo limekabiliwa na mashambulizi kadhaa makubwa ya kigaidi yaliyofanywa na kundi la Al-Shabaab la nchini Somalia, tangu ilipopeleka wanajeshi nchini humo mwaka 2011 kukabiliana na wanamgambo hao.

Idara ya polisi ya kupambana na ugaidi nchini Kenya imeandika katika mtandao wa X kuhusu tishio hilo na kuwaomba Wakenya kuwa waangalifu na kuripoti shughuli zozote za kigaidi ili wachukue hatua.

**DW**

## Wakili feki aliyeshinda kesi 26 akamatwa

**NAIROBI,** KENYA

MTU mmoja aliyejifanya wakili kwa miaka mingi na kushinda kesi 26 mbele ya majaji wa mahakama kuu amekamatwa.

Brian Mwenda, alikamatwa Alhamisi baada ya kikosi cha Chama cha Wanasheria nchini Kenya cha kukabiliana na matukio ya dharura (RAT) kumfuatilia na kubaini anafanya kazi hiyo bila kuwa na taaluma.

Mwenda kwa miaka mingi amefanya kazi ya uwakili katika mahakama kuu ya nchi hiyo bila kuwa na taaluma hiyo, lakini kesi nyingi alishinda.

Kulingana na vyombo mbalimbali vya habari nchini Kenya, wakili huyo feki wakati wote alijitambulisha kama wakili wa Mahakama Kuu na katika hali ya kushangaza kesi 26 alizokuwa akizitetea alishinda.

Ripoti hizo zilieleza kuwa kabla ya kukamatwa, Mwenda alikuwa akisimamia kesi mbele ya Majaji wa Mahakama Kuu na Majaji wa Mahakama ya Rufaa na kushinda zote.

Alikamatwa Alhamisi baada ya Chama cha Wanasheria cha Kenya Tawi la Nairobi Rapid Action Team (RAT) kwa kufanya kazi hiyo bila kuwa na sifa ya taaluma hiyo.

Alikamatwa baada ya timu ya kupambana na vitendo vya dharura kupokea malalamiko kutoka kwa watu mbalimbali kuhusu vitendo vyake vya ulaghai.

Kulingana na rekodi za chama cha wanasheria wa Kenya (LSK), Mwenda si wakili na hana leseni ya kufanya kazi za kisheria nchini Kenya.

Taarifa hiyo ilisema kwamba Mwenda hakuwa wakili wa Mahakama Kuu ya Kenya wala si mwanachama wa LSK Tawi la Nairobi.


Aidha LSK Tawi la Nairobi kupitia timu ya matukio ya dharura (RAT), ilisema mtu huyo amekuwa akijitambulisha na kujifanya kama Wakili wa Mahakama Kuu ya Kenya na mwanachama wa LSK Tawi la Nairobi.

Kwa sasa anazuiliwa katika makao makuu ya timu ya kuchuguza mawakili akisubiri matokeo ya uchunguzi wake kukamilika.

Video za Mwenda zimesambaa mtandaoni akiwa kama wakili akimwakilisha kiongozi wa zamani wa Mungiki katika kesi iliyoonyeshwa kwenye televisheni na kuibua gumzo.

# Zungu ataka vituo tembezi gesi za magari

**Na Joseph Mwendapole**



NAIBU Spika Musa Azzan ameishauri serikali kushirikiana na wamiliki wa vituo vya mafuta kuweka vituo vinavyotembea vya kujaza gesi ili kupunguza msongamano wa magari kwenye vituo vya kujaza gesi.

Amesema kama hilo litafanyika wananchi wengi watachagua kutumia gesi kwenye magari na kuachana na matumizi ya petroli na dizeli ambayo bei yake imeendelea kupaaa.

Zungu alitoa ushauri huo jana wakati akizungumza kwenye hafla ya kutiliana saini baina ya Wakala wa Vipimo (WMA) na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), kuhusu mafunzo ya uanagenzi kwa wanafunzi.

Alisema lazima jitihada zifanyike kuwawekea mazingira mazuri watumiaji wa mafuta ya petroli kuachana na bidhaa hiyo na badala yake watumie gesi ambayo ni rahisi kulinganisha na mafuta.

"Mtungi mmoja wa gesi unaweza kutumia mwezi mzima na kuokoa fedha nyingi sana kulinganisha na petroli na dizeli kwa hiyo serikali itusaidie kwa kushirikiana na wafanyabiashara wa mafuta kupata gesi kwa urahisi kwasababu kwa sasa vituo vya gesi msongamano ni mkubwa watu wanaona kero," alisema Zungu.

Aliwapongeza CBE kwa kutoa mafunzo ambayo yanaendana na soko la ajira na kuwashauri wawe na utaratibu wa kuwatafutia ajira wanafunzi wa chuo hicho kabla hawajamaliza elimu yao chuoni hapo.

Alisema wenye kampuni kubwa nchini hasa za mitandao ya simu wanawataalamu wa hali ya juu ambao ni watanzania na wamekuwa wakiwapata kwa kutembelea vyuoni kuangalia wenye vipaji.

"Mafunzo mnayotoa ni ya hali ya juu kwa hiyo hakuna sababu ya mwanafunzi akamaliza masomo yake hapa akakosa ajira na ninawapongeza kwa ushirikiano ambao mmeuanzisha na WMA kwasababu nafahamu utanufaisha pande zote mbili," alisema Zungu

Zungu pia alikitaka chuo cha CBE kuendelea kujitangaza ndani na nje ya nchi ili kiweze kupata wanafunzi kutoka nchi za kigeni kama ilivyo kwa vyuo vingine kama Chuo cha Afya Muhimbili MUHAS na Taasisi ya Tiba ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), ambayo inapata wagonjwa wengi wa nje ya nchi.

"Hiki chuo nakifahamu miaka mingi sana mko mahiri sana katika kutengeneza wataalamu lakini lazima muongeze nguvu kwenye kitengo chenu cha masoko jitangazeni usiku na mchana dunia ijue kazi mnayofanya na mtapata wanafunzi wengi sana ndani na nje ya nchi," alisema Zungu

Mkuu wa Chuo cha CBE, Profesa Edda Lwoga, alisema kupitia mafunzo ya uanagenzi, wanafunzi wa Shahada ya kwanza ambao wanasoma miaka mitatu watasoma mwaka mmoja na nanusu shuleni na mwaka mmoja na nusu kazini ili wapate elimu ya vitendo itakayowasababisha wawe mahiri kazini.

"Kupitia huu mkataba mwanafunzi wa CBE anayesomea kozi ya vipimo atakuwa anasoma muhula wa kwanza chuoni na muhula wapili anakwenda kufanyakazi WMA ilia pate elimu kwa vitendo na hii kozi ya vipimo inafundishwa na chuo hiki pekee na Afria Mashariki na Kati ni sisi tu tunaotoa kozi hii," alisema

Alisema ili kuendesha kozi hiyo ya vipimo kwa umahiri lazima washirikiane na waajiri na kwamba tayari CBE ilishasaini makubaliano na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili wapate wahitimu ambao wanakubalika sokoni.

Alisema kozi hiyo itatolewa na CBE kuanzia ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada na mwaka huu wa fedha chuo kimeshapata vitendea kazi vya kozi hiyo ambavyo ni mafuta ya petroli, dizeni na mafuta ya ndege na mafuta ya taa vyenye thamani ya milioni 200.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa (WMA), Stela Kahwa, alisema wakala ulikuwa unasubiri siku ya kusaini makubaliano hayo kwa hamu kwani wanamatumaini makubwa ya kunufaika na ushirkiano huo kwa kupata wataalamu bobezi wengi kwenye fani ya vipimo.

Alisema CBE kwa muda mrefu imekuwa ikitoa wataalamu ambao wamekuwa msaada mkubwa kwa WMA na kusema kuwa hata yeye ni matunda ya chuo hicho kwani alihitimu mwaka 1985.

Alisema kazi ya wakala ni kuhakiki vipimo kuhakikisha vinakuwa sawa na hakuna mwananchi anayepunjwa akisisitiza kuwa kwa teknolojia inabadilika kwa kasi basi na mitaala ya vipimo nayo inapaswa kubadilika mara kwa mara kwenda na wakati.

"Kama hufanyi maboresho ya mitaala unaweza kukuta yule ofisa vipimo uliyemfundisha anakuja kwenye soko la ajira vile vipimo ulivyomfundisha havipo kwa sababu hata mimi vipimo vingi nilivyojifunza mwaka 1985 sasa hivi havipo kwa hiyo tusipoboresha mitaala tutapitwa na wakati," alisema

# Maofisa uchunguzi watakiwa kutunza siri za watoa taarifa

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

KATIBU Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Mary Makondo, amewataka maofisa uchunguzi waandamizi kutoka mamlaka mbalimbali za uhifadhi na za kisheria kutunza siri za wananchi wanaotoa taarifa za uhalifu.

Amesema kwa kufanya hivyo kutachangia kuwaondolea woga na kufanikisha kudhibiti matukio ya uhalifu. Makondo aliyasema hayo wakati akizungumza na maofisa uchunguzi waandamizi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS).

Wadau hao wamekutana kwa ajili ya kupitia sheria na kanuni za ulinzi kwa watoa taarifa na mashahidi.

Makondo alisema zinalenga kuimarisha utawala bora na mapambano dhidi ya uhalifu kwa kuwatambua na kuwalinda watoa taarifa na mashahidi na kuwakumbusha kwamba, uadilifu na uaminifu katika utunzaji wa siri ni mujibu wa viapo vyao.

"Kanuni zimefafanua kwa kina kwamba, wale ambao taarifa zao zitafanikisha kuokoa mali ya umma, kupatikana kwa wahalifu na kulinda mazingira na maisha ya binadamu kutokana na uhalifu uliopangwa kufanyika, wamewekewa utaratibu wa kupatiwa motisha," alisema.

Makondo alisema motisha hizo ni pamoja na na kuwafidia wake wote watakaoathirika kutokana na taarifa walizotoa.

Aliwasihi mashahidi kuwa watakapotakiwa kufika mahakamani kutoa ushahidi wasigope kwa kuwa zipo kanuni ambazo zitawalinda dhidi ya changamoto zote za kiusalama.

Mkurugenzi Msaidizi wa Ufuatiliaji Haki wizarani hapo, Beatrice Mpembo, waliowezeshwa kutunga kanuni za ulinzi kwa watoa taarifa na mashahidi na washirika wa maendeleo serikali ya Uingereza FCDO na Umoja wa Ulaya, kupitia program endelevu ya kupambana na rushwa BSAAT, kutoka Ofisi ya Rais, Ikulu, alisema lengo la sheria hiyo ni kuimarisha utawala bora na mapambano dhidi ya uhalifu.

Alisema zitarahisisha utekelezaji wa sheria husika kuwa yenye tija na ufanisi mkubwa ili kuwezesha haki kutendeka kwa wakati katika jamii na kutoa ulinzi wa kisheria kwa watoa taarifa za uhalifu wa makosa mbalimbali.

Mratibu wa Program Endelevu ya Kupambana na Rushwa, BSAAT, kutoka Ofisi ya Rais, Ikulu, Dk. Boniventure Baya, aliipongeza wizara hiyo kwa namna wanavyogusa makundi muhimu kuifahamu sheria na kanuni hizo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI IRINGA**
**SHAURI LA MADAI NA.01/2023**
**MUCOBA BANK PLC...............MDAI**
**DHIDI YA**
**CYNTHIA MEMES MTUI.........WADAIWA**
**KIGUNGA G. MWANGWA**

**KUITWA SHAURNI**

Shauri tajwa hapo juu limepangwa kutajwa tarehe 19 Oktoba,2023 saa mbili na Nusu (8:30) asubuhi, hivyo wadaiwa katika shauri hilo wanatakiwa kufika katika mahakama ya hakimu mkazi Iringa ama kutuma wawakilishi wao.

Fahamu kuwa endapo kama wahusika hawatofika siku hiyo au kutuma wawakilishi wao, shauri hilo litapangwa tarehe ya kusikilizwa upande mmoja bila wao kuwepo.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI
IRINGA.

**KUPOTEA KWA CHETI**



ROSEMARY CHARIES LUGWISHA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index No. S00771/0054/2017 kilichotolewa na baraza la Mitihani kupitia ASKOFU ADRIAN MKOBA mwaka 2017.Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa polisi: PHQ/DOD/DOD/3542/2023.

**KUBADILISHA JINA.**

NIMEBADILISHA JINA LANGU KUTOKA ATUL MOVALIYA NA KUWA ATUL PRAGJIBHAI MOVALIYA NA KWA SASA NITAJULIKANA KWA JINA JIPYA AMBALO SAHIHI: ATUL PRAGJIBHAI MOVALIYA.
ANUANI: A1, 1ST FLOOR, YOGI SADAN APARTMENT, KISUTU DAR ES SALAAM, TANZANIA
[KWA MADHUMUNI YA KUHUISHA PASIPOTI]

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 118 YA 2023**
**ELINA ELIMBORA KIMARO .........MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**JULIET GABRIEL NJOVU................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA; JULIET GABRIEL NJOVU**
Popote Ulipo Unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 08/11/2023 mbele ya Mwenyekiti M.KHASIM wewe mwenyewe binafsi au mtume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 12 mwezi October , 2023.

.... M. KHASIM MWENYEKITI ....

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No 99 of 2023**
**In the Matter of the Estate of the Late SOLOMON SAMSONI MUNUO Of Makole within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by BI FAUSTINA SOLOMONI MUNUO**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 01 day of 11......................... 2023
Dated at Dodoma this 11 day of 10....................2023

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE I/C
DODOMA DISTRICT

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**LAURENT STEVEN GUNDULA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 268 DEC – BOXER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/23565/2023**

**KUPOTEA KWA CHETI**




**YOHANA EDWARD SHOO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha ne chenye index namba **S.0658/0059** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MWAMAPALALA SECONDARY SCHOOL** Mwaka 2003. Kwa yeyote atakaeona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **MB/RB/7462/2007**

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

# Maiti kwenye kiroba-30

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




"Bwana Frank, kilichotokea kwenye kesi hii ambacho mimi nimekipeleleza ni kwamba, kuna dada mmoja anaitwa Rukia. Alisoma na marehemu Tessy. Charton aliwafahamu na kutokea kumpenda Tessy kiasi cha kumuoa. Lakini ndani ya moyo wake Rukia yeye alimpenda Charton. Ikakaa akilini mwake kuwa ipo siku ataisambaratisha ndoa na Charton atangia mikononi mwake.

Katika pitapita zake akafanikiwa kupata picha ya mwanaume mmoja aliyepiga na Tessy miaka mingi sana nyuma. Mwanaume huyo ni kweli alikuwa mpenzi wa Tessy kabla ya kukutana na Charton. Na yeye mwenyewe Rukia anamfahamu. Mtu huyu anaitwa Barton. Kwa sasa nasikia anaishi nchini Uingereza.

Rukia aliipeleka kwa makusudi na kumuonyesha Charton ambaye naye bila kuhoji au kutafakari akaamini kuwa mkewe anamsaliti.

Ukweli ni kwamba picha ile ilipigwa zamani, Charton akadanganywa kuwa ni mpya.

Na kilichomuaminisha zaidi kuwa ilikuwa mpya ni wajihi wa mkewe. Alimkuta akiwa mwembamba sana kutokana na maisha yaliyokuwa anaishi kipindi hicho.

Sasa ile picha afande alionekana amenawiri kama ilivyo sasa kwa hiyo jamaa akajua haikupigwa muda mrefu sana. Kumbe Tessy kabla maisha hayajampiga kwa kuchana na mwanaume wake Barton alikuwa mrembo kama alivyokuwa kabla ya kuuawa."

Inspekta Frank kwa muda mfupi alipoanza kumsikiliza Eddy aligundua kuwa ni kisa kikubwa chenye ushahidi uliofunganama na ni kweli ilitakuwa kuwe na mpelelezi mwenye akili ya ziada kuweza kukitatua.

"Wakati Rukia akidhania kuwa Tessy ataachwa kwa kupewa talaka ili aolewe yeye, Charton alikuwa na mawazi tofauti kidogo.

Kwanza hakumwambia mtu yoyote. Hata hawenda kumuuliza mkewe. Badala yake alikaa na hasira moyoni. Alichoamua ni kuwaua wote wawili. Mkewe na hawara yake. lakini Barton hakupatikana kwa sababu miaka mingi alikuwa ameshakwenda Uingereza.

Akapanga kumuua mkewe kutokana na wivu mkali aliokuwa nao. Lakini akajua kabisa ni lazima awe makini kama anataka kufanya hivyo ili asiingie kwenye mkono wa sheria. Na hata kitendo cha kutomwambia mkewe au yoyote ile ilikuwa ni kutowapa pa kuanzia polisi

**"Kumbe aliwapoteza watu maboya, alipanda ndege siku hiyo hiyo na kutua Dar. Huku alikuwa anawasiliana na Patauli kwa maneno ya mafumbo, au kiswahili ambacho walipangana na kuelewana wenyewe amsake mkewe, amkamate na kumpeleka kwenye nyumba ile ya Banana.**

upelelezi atakapofanya mauaji.

Akamtafuta jambazi Tinga Patauli ambaye alimlipa pesa kwa kazi moja ya kumuongoza kumtesa mkewe na kumuua kwa mateso makali."

"He! Ndivyo ilivyokuwa?" Akahoji Inpekta Frank.

"Jamaa alivyokuwa anajua kutengeneza mazingira ya kufuta nyayo au ushahidi, alianza kumpa nitosi mpangaji wake wa nyumba aliyoipangisha maeneo ya Banana kwa Mapunda.

Akamhamisha na nyumba hiyo ikabaki bila mpangaji kwa muda mrefu, lengo ilikuwa ni kupata eneo la kumtesa na kumuua mkewe.

Charton ni mfanyakazi ya Idara ya Maliasili anayeishi Dar es Salaam na kufanya kazi Dodoma.

Mpango wake waliuandaa kiufundi sana, kwani baada ya kwenda Dodoma yeye na wafanyakazi wenzake walipata safari ya kwenda semina jijini Mwanza. Ilikuwa ya siku tatu. Baada ya kumaliza wenzake walipanda basi na kurejea Dodoma. Yeye akawaambia wenzake anabaki jijini Mwanza, wenzake wakajua tu amepata mpenzi ambaye anataka kukesha naye japo usiku mmoja au siku mbili."

Afande Frank aliendelea kuwa kimya akishangaa umahiri aliyoufanya Eddy katika kufuatilia suala hilo ambalo awali ilionekana kama ni kama mauaji ya Tessy yaliyofanya na watu wengine kabisa ambao hawana uhusiano naye. Kumbe ni mumewe kabisa wa ndoa.

"Kumbe aliwapoteza watu maboya, alipanda ndege siku hiyo hiyo na kutua Dar. Huku alikuwa anawasiliana na Patauli kwa maneno ya mafumbo, au kiswahili ambacho walipangana na kuelewana wenyewe amsake mkewe, amkamate na kumpeleka kwenye nyumba ile ya Banana.

Charton na mkewe walikuwa wakiishi Gongolamboto. Kwa maana hiyo haikumuwia tabu Patauli kumteka Tessy mpaka Banana na kumuweka kwenye nyumba ile.

Charton alitua Uwanja wa Ndege Julius Nyerere Dar es Salaam na kwenda moja kwa moja Banana akaungana na Patauli, kumtesa mkewe, kumuonyesha picha za yule mpenzi wake wa zamani Burton, kumuuliza maswali ya kipuuzi, wakamfanyia ukatili mkubwa, wakaanza kumkatakata viungo wakati hupo hai. Shahidi wa hili ni Mboneka Fisimaji, mpwa wa Patauli ambaye yeye alichukuliwa kwa ajili ya kubeba furushi la maiti. Hakuna yoyote aliyejua hili. Kila mmoja, ndugu jamaa na marafiki walijua Charton yupo kikazi Dodoma."

Alichokuwa akikisikia Inspekta Frank kutoka kwa Eddy ni kama muvi anazoziona kwenye televisheni, lakini leo anaona na kusikia kisa hiki laivu kimetokea bongo.

"Kwa kukukumbusha tu afande ni kwamba kule Mwanza alikokaa Charton alimtafuta mtu mmoja na mpenzi wake kabla hajasafiri, akawapeleka kwenye hoteli moja maarufu, akawalipa na pesa, mwanaume akatumia jina lake na kukaa na mwanamke huyo kwa siku mbili.

Lengo ni kama kutakuwa na kusaka ushahidi basi ionekane alikuwa jijini Mwanza kwa siku mbili, hivyo wakati mkewe anapotea na maiti yake kugunduliwa kwenye kiroba alikuwa jijini Mwanza.

Kusema kweli huyu jamaa ni mzuri sana kwenye kuficha ushahidi. Bahati mbaya tu amekutana na mimi, vingi-

ITAENDELEA JUMAPILI

# JKU, KVZ HAPATOSHI LIGI KUU ZANZIBAR LEO

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MAAFANDE wa JKU wanatarajia kukutana na wenzao kutoka KVZ SC katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kuanzia saa 10:15 jioni kwenye Uwanja wa Mau A.

Timu hizo zitakutana kila mmoja akiwa na pointi 13 baada ya kushinda mechi nne na kutoka sare mara moja na kuufanya mchezo wa leo kutabiriwa kuwa na ushindani.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa KVZ, Ali Mohammed alisema amekiandaa vyema kikosi chake na anatarajia watacheza bila ya hofu au papara katika mchezo huo.

Mohammed alisema katika siku tatu za mapumziko walizopata ametumia muda mwingi kufanya mazoezi ya kuwajenga wachezaji kisaikolojia ili kutokuwa na wasiwasi kwa sababu anahitaji kupata pointi tatu muhimu.

Kocha huyo alisema anajua anaenda kukutana na timu ngumu ambayo inahitaji kushinda mchezo huo na malengo yao yanafanana.


"Kikosi mpaka sasa kipo vizuri, sina majeruhi ambao wanaweza kuukosa mchezo, wachezaji wangu wote wa kikosi cha kwanza watakuwapo uwanjani, ninahakika tunawafurahisha mashabiki wetu kwa kushinda mchezo huu," alisema kocha huyo. Naye Kocha Mkuu wa JKU, Salum Ali alisema anashuka uwanjani akiwa na lengo moja la kushinda mchezo huo na kubakia kileleni katika msimamo wa ligi hiyo yenye kushirikisha timu 16.

Alisema kuelekea mchezo huo kama mwalimu hana hofu kubwa licha ya mashabiki na wadau wa soka visiwani kuiona mechi hiyo itakuwa na ushindani mkubwa kutokana kulingana kila kitu.

"Lengo letu kuu katika msimu huu ni kuhakikisha tunapata alama tatu ama tuwe ugenini au nyumbani, tunashuka dimbani kwa lengo moja tu la kupata ushindi na sio vinginevyo, tayari wachezaji wanahamasa kubwa na wapo vizuri kuhakikisha tunatimiza malengo," alisema kocha wao.

Wakati huo huo, Ngome imeendelea kuwa na msimu mbaya baada ya kupokea kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Kipanga katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A juzi jioni.

Bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar ambayo inadhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), atapata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.




Ofisa Mkuu wa Biashara wa Kampuni ya SANLAM, Kyenekiki Kyando (kulia), akimkabidhi tiketi ya ndege mshindi wa mbio za CRDB Marathon, Nestory Stephen aliyeondoka nchini jana kuelekea Afrika Kusini kushiriki mashindano ya mbio ndefu. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Stephen aahidi medali bondeni

**Na Joseph Mwendapole**

MSHINDI wa mbio za CRDB Marathon, Nestory Stephen ameahidi kufanya vyema katika mbio za Cape Town SANLAM International Marathon zitakazofanyika kesho nchini Afrika Kusini.

Mwakilishi huyo wa Tanzania aliondoka nchini jana baada ya kukabidhiwa tiketi ya ndege na Kampuni ya SANLAM ambao ni wadhamini wenza wa mbio za CRDB Marathon.

Akizungumza na gazeti hili kabla ya kuondoka, Nestory alisema amefurahi kupata fursa hiyo na matarajio yake atafanya vizuri na kuiwakilisha vyema Tanzania katika mashindano hayo.

"Nawaahidi Watanzania wenzangu nitafanya vizuri kwa sababu nimefanya mazoezi ya kutosha, naamini nitafanya vizuri, sitawaangusha," alisema Nestory.

Mkuu wa Uendeshaji wa CRDB Foundation, Joycelean Makule alisema mshindi huyo amepewa fedha na SANLAM ili kuwa katika nafasi ya kufanya vyema katika mbio hizo kubwa kuliko zote Afrika.

"Mshindi amepewa tiketi, hela ya matumizi na atahudumiwa malazi akiwa Afrika Kusini kwa ajili ya kushiriki mbio hizo za kimataifa zijulikanazo kama Cape Town SANLAM International Marathon, anakwenda kuiwakilisha nchi yetu," alisema Makule.

Alieleza mshindi huyo alipatikana katika mbio za CRDB Marathon zilizofanyika Agosti, mwaka huu na yeye kuibuka kinara katika umbali wa za wa kilomita 42.

## Kuogelea walemavu kuchuana Gymkhana

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO maalumu ya kuogelea kwa watu wenye ulemavu yamepangwa kufanyika leo kwenye Bwawa la Gymkhana jijini, Dar es Salaam imeelezwa.

Katibu Mkuu wa Chama cha Kuogelea kwa watu wenye ulemavu Nchini (TPSA), Ramadhani Namkoveka alisema mashindano hayo yanafanyika kwa mara ya kwanza nchini na yatashirikisha waogeleaji 82 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

"Maandalizi kuelekea mashindano hayo yanaendelea vizuri, tunazishukuru taasisi ambazo zimetuunga mkono ili kufanikisha malengo yetu," alisema Namkoveka.

Katibu huyo alisema lengo la TPSA kundaa mashindano hayo ni kupata wachezaji watakaounda Timu ya Taifa itayoshiriki michuano mbalimbali ya kimataifa hapo mwakani.

Alisema waogeleaji watakaoteuliwa kuunda timu hiyo watapa fursa ya kushiriki mafunzo ili kuimarisha afya pamoja na miili yao na aliongeza kwa kuwaomba wadau wajitokeze kushuhudia vipaji katika mashindano hayo.

## Polisi, SBL waandaa Usalama Jamii CUP

**Na Frank Monyo**

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kushirikiana na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), wanatarajia kuanzisha mashindano ya soka yatakayojulikana kama 'Usalama Barabarani Jamii Cup 2023' ambayo yatashirikisha waendesha pikipiki wa Mkoa wa Dar es Salaam, imeelezwa.

Kamanda wa Polisi Usalama wa Barabarani, Ramadhani Ng'azi alisema jana Idara ya Trafiki inalenga kukuza usalama barabarani, kwa kudhibiti uendeshaji wa vyombo vya moto bila kutumia vilevi.

"Tuna dhamira kubwa ya kufanya barabara zetu kuwa salama zaidi kwa kukuza tabia za kunywa kwa uwajibikaji, tunatarajia kufanya kazi kwa bidii kufikia malengo haya. Kampeni ya INAWEZEKANA inaonyesha dhamira kuu ya SBL katika jukumu lake la kijamii na ustawi wa wateja wake na jamii kwa ujumla," Ng'azi alisema.

Naye Mkurugenzi wa Ubunifu na Masoko wa SBL, Anitha Rwehumbiza alisema ushirikiano huo ni hatua ya kampuni yao kuendelea kutoa elimu kwa watumiaji wa vyombo vya moto kunywa kistaarabu kupitia kampeni ya INAWEZEKANA.

"Ushirikiano huu wa SBL na Jeshi la Polisi unalenga kushirikisha waendesha pikipiki na wapenzi wa mpira wa miguu katika ngazi zote za mashindano, kuanzia ngazi za kata hadi kitaifa," alisema Rwehumbiza.

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS ANUKIA BAYERN

MABINGWA wa Ujerumani, Bayern Munich wanafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Manchester City na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 27 ifikapo Januari, huku kocha, Thomas Tuchel akitumaini kuimarisha safu ya kati ya timu yake. **(Sun)**

### KROOS ATAKIWA CITY

MANCHESTER City imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Real Madrid na Ujerumani, Toni Kroos mkataba wake utakapomalizika msimu ujao wa joto, huku City wakiwa tayari kumlipa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 mshahara wa pauni milioni 13 kwa msimu. **(Mundo Deportivo)**

### SMITH ATAJWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imemworodhesha kiungo wa kati wa Arsenal na Timu ya Taifa ya England, Emile Smith Rowe mwenye umri wa miaka 23 katika mipango ya kumsajili Januari. **(Express)**

### WILSHERE ANUKIA MAREKANI

KOCHA mkuu wa Timu ya Vijana ya umri chini ya miaka 18 ya Arsenal, Jack Wilshere yuko katika mazungumzo ya kutua katika klabu inayoshiriki Ligi Kuu ya Soka ya Marekani, Colorado Rapids. **(Telegraph)**

### OLMO AGOMBEWA ULAYA

KLABU ya Manchester City inaongoza katika mbio za kumsaka fowadi wa RB Leipzig na Hispania, Dani Olmo mwenye umri wa miaka 25, huku Real Madrid, Arsenal na Chelsea zIkimwania pia nyota huyo. **(Mundo Deportivo, via Goal)**

### WAARABU WAMTAKA ZOUMA

BEKI wa West Ham United na Ufaransa, Kurt Zouma (28), analengwa na klabu ya Saudi Arabia. Wagonga nyundo hao wamemtambua beki wa kati wa Manchester United na England, Harry Maguire (30), na mlinzi wa Bayer Leverkusen, Edmond Tapsoba (24) kama wachezaji wanaotarajiwa kuchukua nafasi yake. **(90 min)**

### BOSI SAUDIA NA SALAH

MKURUGENZI wa Soka wa Saudi Pro League, Michael Emenalo amemtaja mshambuliaji wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 31, kuwa ni “kipenzi chake kibinafsi” zaidi. **(Metro)**

### VERMEEREN AGEUKA LULU

KLABU z Manchester City, Arsenal na Tottenham Hotspur zote zimewasiliana na Royal Antwerp kuhusu kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya vijana ya Ubelgiji (U-21), Arthur Vermeeren. **(90min).**

### UNITED, CHELSEA VITANI

MANCHESTER United, Chelsea na Bayern Munich zote zinamfuatilia kiungo wa kati wa Schalke, Assan Ouedraogo mwenye umri wa miaka 17. **(Team Talks)**

### PAQUETA MAMBO SAFI

KLABU ya West Ham inataka kumfunga kiungo wa kati wa Brazil, Lucas Paqueta mwenye umri wa miaka 26 kwa kumpa mkataba mpya. **(Mail)**

### BUCK AINGIA SOKONI

KLABU za Manchester City, Arsenal na Burnley zinataka kumsajili kiungo wa kati wa New England Revolution na England, Noel Buck mwenye umri wa miaka 18. **(Athletic)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ROONEY: NITAIREJESHA BIRMINGHAM LIGI KUU

Ni kauli ya kocha huyo mpya ambaye ametua katika...

**BIRMINGHAM, England**

WAYNE Rooney anapanga kikamilifu kuirejesha Birmingham City katika Ligi Kuu ya England (EPL), baada ya kuteuliwa kuwa kocha mkuu wa klabu hiyo.

Nahodha huyo wa zamani wa Manchester United na England alitangazwa kurithi mikoba ya John Eustace Jumatano iliyopita, siku chache baada ya kuachana na timu inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani, DC United.

Katika mkutano wake wa kwanza na waandishi wa habari kama kocha, Rooney hakuficha matamanio yake makubwa kwa kuirejesha timu hiyo kwenye Ligi Kuu England baada ya miaka 12 tangu ishuke daraja.

Rooney mwenye umri wa miaka 37 alisema: “Hilo ndilo lengo, kurudisha klabu hii kwenye Ligi Kuu bila shaka ndivyo ilivyo. Kuna kazi nyingi za kufanywa katika klabu nzima ya soka. Lakini Ligi Kuu ndio tunataka kufika.

Ni matarajio yangu, ni matarajio ya klabu na tunaweka kila kitu ili kuhakikisha tunafanya hivyo katika siku za usoni.” Rooney alisema.

Rooney, ambaye alianza safari yake ya ukocha kwa muda wa miaka miwili katika klabu ya Derby kabla ya kwenda Marekani, alifichua alikataa ofa kutoka kwa klabu nyingine za England ili kujiunga na timu hiyo.

Aliongeza: “Kurejea katika soka la Uingereza ni jambo kubwa. Ni wazi ni kitu ambacho nimekuwa nikitaka kufanya na kusema ukweli, nimepata nafasi ya kufanya hivyo katika kipindi cha wiki nne hadi sita zilizopita katika klabu nyingine.

“Lakini tangu kuzungumza na Birmingham na kuona nia ya klabu na wapi wanataka kwenda, ilinisisimua.

“Nataka kupata mafanikio na ni wazi klabu inataka kuwa na mafanikio. Kila kitu tulichozungumza kilikuwa sawa sana kwa hiyo ulikuwa uamuzi rahisi mara tu nilipozungumza nao.

“Nilifanya mazoezi yangu ya kwanza na wachezaji na itakuwa tofauti kidogo na walivyozoea lakini ni wakati wa kusisimua na nina furaha kuwa sehemu yake.”

Mechi ya kwanza ya Rooney dimbani itakuwa dhidi ya Middlesbrough, ambayo inanolewa na mchezaji mwenzake wa zamani wa United, Michael Carrick itachezwa Oktoba 21, mwaka huu.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,161,7

MECHI KALI
USA
VERSUS
GERMANY
1 | 3.65
X | 3.80
2 | 1.91

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
airtel money EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MBAPPE AITWA MADRID KUJIUNGA NA BELLINGHAM

**MADRID, Hispania**

MJUMBE wa Bodi ya Real Madrid, Jose Manuel Otero Lastre amemhimiza, Kylian Mbappe ajiunge na Jude Bellingham huko Santiago Bernabeu.

Mbappe mwenye umri wa miaka 24, amekuwa akihusishwa sana kuhamia kwa Los Blancos baada ya kuashiria nia yake ya kuondoka Paris Saint-Germain mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

Bellingham amekuwa na kiwango bora tangu alipoondoka Borussia Dortmund na sasa Otero Lastre anataka Mbappe aige mfano huo.

Alikiambia Kituo cha Remontada Blanca Twitch: "Tunatumaini Mbappe ana mawazo sawa na Bellingham.

"Ninaamini atakuja. Mbappe atapata utukufu atakapokuja Real Madrid. Atashinda Ligi ya Mabingwa Ulaya siku moja.

"Sasa, inaonekana kama PSG hawana nguvu zaidi kuliko hapo awali kwa sababu hawana tena wachezaji wazuri kama hao.

"Madrid inahakikisha usalama, umakini unaoleta matokeo. Ninaamini atasema ndiyo wakati akiwa mchezaji huru. Mbappe alizaliwa kuichezea Real Madrid."

Mbappe alikaribia kujiunga na Real msimu wa joto lakini Otero Lastre aliendelea kueleza kwa nini mpango uliopendekezwa haukutimia.

Aliongeza: "Mbappe hakuwa na fursa ya kusaini Real Madrid msimu huu wa joto.

"Ili kuja, angelazimika kuacha mafao ya juu sana ambayo tayari alikuwa amekubaliana na Paris Saint-Germain.

"Kiasi ambacho kingelipwa ili kumsajili Mbappe mwaka mmoja mapema kilikuwa cha kichaa.



# Wilshere anukia Colorado Rapids

**COLORADO, Marekani**

COLORADO Rapids imefanya mahojiano na Kocha wa Timu ya vijana ya Arsenal na kiungo wa zamani, Jack Wilshere kuhusu nafasi iliyo wazi ya kocha mkuu wa klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani (MLS), kwa mujibu wa ESPN.

Rapids inamilikiwa na Kroenke Sports & Entertainment, ambao pia wanaimiliki Arsenal, na sasa inafanya mazungumzo na Wilshere mwenye umri wa miaka 31.

Wilshere alistaafu kucheza mwaka jana lakini ameanza vyema maisha yake ya ukocha, na kukiongoza kikosi cha Arsenal chini ya umri wa miaka 18 kutinga fainali ya Kombe la FA katika msimu wake wa kwanza.

Vyanzo viliiambia ESPN Wilshere anafuraha Arsenal, lakini ana nia ya kuhamia katika nafasi ya usimamizi wa juu zaidi na sasa anasubiri kusikiliza ofa ya klabu hiyo ya MLS.

The Rapids kwa sasa wako mkiani mwa Ligi ya Ukanda wa Magharibi ya MLS baada ya kuachana na kocha mkuu, Robin Fraser mwezi uliopita.



95,478/-

# MASHUJAA YATAMBA IKO IMARA LIGI KUU 2023/24

Na Saada Akida

IKICHEZA mechi tazo za Ligi Kuu Tanzania Bara, Klabu ya Mashujaa imesema inaridhishwa na mwenendo wa timu yake ambayo inashiriki kwa mara ya kwanza ligi hiyo.

Mashujaa iko katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa imejikusanyia pointi nane baada ya kushinda mechi mbili na sare mbili.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Mashujaa, Mohammed Abdallah 'Bares' alisema anaamini timu yake itaendelea kupambana ili kusaka matokeo bora na hatimaye kufikia malengo.

Hata hivyo Bares alisema timu yake bado haina uwezo wa kumaliza katika nafasi mbili za juu katika ligi hiyo ambazo zinatolewa 'macho' na vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga.

Kocha huyo alisema kikosi chake kina uwezo wa kumaliza msimu katika nafasi ya tatu au ya nne endapo wachezaji wake wataendelea kujituma na kupambana.

"Ligi ni ngumu lakini hatupaswi kuacha kuweka mikakati yetu, awamu ya kwanza ya mechi tano tumefanikiwa na sasa mechi tano za awamu ya pili tukusanye alama zote 15 au nane kama tulivyofanya awamu ya kwanza.

Katika kuhakikisha tunafanikiwa malengo yetu, tunalazimika kutafuta matokeo chanya kila mechi, ikiwa tunacheza ugenini au nyumbani, kwa sasa tunajiandaa dhidi ya Coastal Union, baada ya hapo tunaangalia ratiba kama tutacheza na Simba au nani," alisema kocha huyo.

Aliongeza licha ya Coastal Union kuanza vibaya msimu, wao hawatabweteka na watajiimarisha ili kuwavaa mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara mwaka 1988.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 15, wakifanya mazoezi ili kujiandaa na mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-15) yatakayofanyika Kenya hivi karibuni. **PICHA: TFF**

## Simba SC, Yanga

INATOKA UK. 24

kuelekea katika mechi ya ufunguzi wa michuano ya AFL kwa kuandaa Simba Beach Bonanza litakalofanyika kwenye ufukwe wa Coco, jijini Dar es Salaam.

Timu ya Kamati ya Roho Mbaya itacheza mechi ya kwanza dhidi ya dhidi ya Karume Unstoppable wakati Nguvu ya Simba Asili itakutana na Wekundu wa Terminal huku Simba Ushirikiano ikicheza dhidi ya Simba Makao Makuu Whatsapp Group.

Mechi nyingine itakuwa ni kati ya Mpira Pesa Mikumi dhidi ya Wekundu wa Mtongole, Asili ya Simba dhidi ya Wekundu wa Kariakoo na Simba Platinum itavaana na Simba Vibes.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema anafanyia kazi makosa mbalimbali yaliyojitokeza katika mechi walizocheza ili kurejea katika ligi hiyo wakiwa imara zaidi.

"Tunahitaji kuwa imara zaidi, kila timu inajipanga kusaka ushindi, hakuna mechi rahisi, muda huu wa mapumziko ni wa kujiimarisha katika kila idara, " Gamondi alisema kwa kifupi.

## Stars yapewa nafasi AFCON

INATOKA UK. 24

yao imepangwa katika kundi gumu kwa sababu kila nchi iliyoingia kwenye fainali hizo ni lazima ikutane na 'mkubwa' mwenzake.

"Tulitaka tupangwe na Djibouti au Somalia? Huku hao hawapo, kuna timu kubwa ngumu ambazo hata sisi tunazimudu pia. Tanzania tumeshatoka huko, hebu angalia hata kwenye klabu zetu, Simba imeingia makundi na robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika mara nne sasa, Yanga msimu uliopita ilifika fainali ya Kombe la Shirikisho.

Tuna wachezaji wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi, hata hao Algeria hivi karibuni tulitoka nao sare kwao, hivyo sidhani kama kuna haja ya kuogopa kundi kwa sababu Tanzania kwa sasa ni moja kati ya nchi kubwa kwenye soka," alisema Julio.

Beki huyo alisema hata kwenye uongozi wa soka nchini kwa sasa kuna safu ya wanamichezo halisi ambao wamekuwa karibu katika kusaidia masuala mbalimbali wakiongozwa na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, Naibu wake, Hamis Mwinjuma 'Mwana FA' na Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Leodegar Tenga, ambaye aliwahi kuichezea Stars kwa mafanikio.

Selemani Matola nahodha na kiungo wa zamani wa Simba aliliambia gazeti hili mechi ngumu kwa Stars ni dhidi ya Morocco na wapinzani wengine waliobakia wanawamudu.

"Sio kundi gumu kama watu wengi wanavyodhani kama tukijiandaa vizuri, sidhani kama wachezaji wetu wana woga na wachezaji wa timu hizo kwa sababu wanakutana nao sana kwenye ngazi ya klabu. Mimi binafsi, ukiiondoa Morocco, Tanzania ina uwezo wa kuziadhibu zilizobaki na kusonga mbele, tuna kila kitu kwa sasa, tuna wachezaji wengi wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi wenye uwezo mkubwa na hata wa ndani, niseme tu, Zambia na DRC tunazimudu," alisema mchezaji huyo wa zamani wa Stars.

Fainali za AFCON zimepangwa kufanyika kuanzia Januari 13 hadi Februari 11, mwakani nchini Ivory Coast.



## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/10/23 | 19:30 | Sporting Gijon vs Real Zaragoza | 2.12 | 3.00 | 3.65 |
| 02. 14/10/23 | 19:30 | FC Cartagena vs Racing Santander | 2.24 | 3.05 | 3.25 |
| 03. 14/10/23 | 21:45 | Hungary vs Serbia | 2.42 | 3.05 | 2.65 |
| 04. 14/10/23 | 23:00 | Ituano vs CR Brasil | 2.30 | 2.95 | 3.25 |
| 05. 14/10/23 | 23:00 | Detroit City vs Pittsburgh Riverhounds | 2.65 | 3.40 | 2.25 |
| 06. 15/10/23 | 00:00 | Deportivo Pereira vs La Equidad | 2.15 | 3.05 | 3.05 |
| 07. 15/10/23 | 02:05 | Alebrijes de Oaxaca vs Cancun | 2.21 | 3.20 | 2.85 |
| 08. 15/10/23 | 02:10 | Atletico Nacional vs Independiente Medellin | 2.13 | 3.10 | 3.05 |
| 09. 15/10/23 | 03:00 | Cuiaba vs Cruzeiro | 2.35 | 3.05 | 3.05 |
| 10. 15/10/23 | 05:00 | Monterey Bay vs Orange County | 2.16 | 3.40 | 2.75 |
| 11. 15/10/23 | 05:30 | Las Vegas Lights vs San Diego Loyal | 2.85 | 3.40 | 2.11 |
| 12. 15/10/23 | 05:30 | LA Galaxy vs Real Salt Lake | 2.25 | 3.65 | 2.50 |
| 13. 15/10/23 | 08:00 | Osaka vs Gifu | 2.75 | 2.90 | 2.43 |
| 14. 15/10/23 | 17:15 | Eldense vs Elche | 3.30 | 3.05 | 2.22 |
| 15. 15/10/23 | 17:30 | Preussen Munster vs 1860 Munich | 2.17 | 3.35 | 2.75 |
| 16. 15/10/23 | 21:30 | CA Estudiantes vs Tristan Suarez | 2.20 | 3.30 | 3.10 |
| 17. 15/10/23 | 21:45 | Ponte Preta vs AC Goianiense | 3.10 | 2.90 | 2.40 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 14/10/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5054 | KamAZ vs Shinnik Yaroslavl | 2.15 | 3.03 | 3.18 |
| 14:30 | 1169 | Notts County vs Mansfield | 2.13 | 3.53 | 2.89 |
| 15:00 | 1219 | Unterhaching vs Sandhausen | 2.58 | 3.36 | 2.54 |
| 15:00 | 2421 | Jahn Regensburg vs VfB Lubeck | 1.73 | 3.68 | 4.35 |
| 15:00 | 2466 | Osmanlispor vs Kirklarelispor | 1.42 | 4.17 | 6.31 |
| 15:00 | 3385 | Wolkite City FC vs Sidama Bunna SC | 2.63 | 2.94 | 2.63 |
| 15:00 | 3777 | Verl vs Ingolstadt | 2.23 | 3.57 | 2.84 |
| 15:00 | 4588 | Viktoria Koln vs Erzgebirge Aue | 1.96 | 3.57 | 3.47 |
| 15:00 | 5299 | Ankara Demirspor vs Bucaspor | 3.02 | 3.07 | 2.26 |
| 15:30 | 3858 | Altinordu vs Serik Belediyespor | 1.75 | 3.40 | 4.27 |
| 15:30 | 4281 | Denizlispor vs Inegolspor | 2.02 | 3.25 | 3.35 |
| 16:00 | 1364 | Ukraine vs North Macedonia | 1.64 | 3.75 | 5.49 |
| 16:00 | 1382 | Sloboda vs FK Radnicki Beograd | 1.71 | 3.17 | 4.74 |
| 16:00 | 2969 | Green Buffaloes vs Power Dynamos | 4.85 | 2.88 | 1.80 |
| 16:00 | 5650 | FC Muza vs Forest Rangers | 1.80 | 3.03 | 4.44 |
| 16:00 | 5940 | Wurzburg vs SV Fortuna Regensburg | 2.15 | 3.60 | 2.79 |
| 17:00 | 1430 | Grimsby vs Accrington | 2.01 | 3.34 | 3.29 |
| 17:00 | 1479 | Port Vale vs Fleetwood Town | 2.17 | 3.31 | 3.16 |
| 17:00 | 1569 | Blackpool vs Stevenage | 2.31 | 3.30 | 2.90 |
| 17:00 | 1572 | Cambridge Utd vs Shrewsbury | 2.05 | 3.35 | 3.40 |
| 17:00 | 2271 | Rayo Majadahonda vs CE Sabadell | 2.79 | 2.94 | 2.49 |
| 17:00 | 2427 | Lincoln vs Burton | 1.94 | 3.35 | 3.75 |
| 17:00 | 2725 | Carlisle vs Leyton Orient | 2.42 | 3.24 | 2.80 |
| 17:00 | 4119 | MK Dons vs Barrow | 2.00 | 3.33 | 3.33 |
| 17:00 | 5216 | Forest Green vs Colchester | 2.36 | 3.34 | 2.65 |
| 17:15 | 3896 | Mirandes vs Tenerife | 3.02 | 2.92 | 2.40 |
| 17:30 | 1222 | Arminia Bielefeld vs Waldhof Mannheim | 2.06 | 3.52 | 3.21 |
| 17:30 | 1315 | Urozhay Krasnodar vs Torpedo Moscow | 2.78 | 3.03 | 2.38 |
| 17:30 | 1784 | VVV Venlo vs Roda Kerkrade | 2.37 | 3.47 | 2.60 |
| 17:30 | 2025 | USM Alger vs USM Khenchela | 1.80 | 3.06 | 4.58 |
| 18:00 | 1961 | Longford Town vs Bray Wanderers | 3.12 | 3.53 | 1.98 |
| 18:00 | 3911 | FK Khimki vs Yenisey Kr | 1.87 | 3.32 | 3.63 |
| 18:00 | 4150 | Welayta Dicha FC vs Adama City FC | 2.65 | 2.75 | 2.65 |
| 19:00 | 2375 | Slovenia vs Finland | 1.89 | 3.27 | 4.43 |
| 19:00 | 4853 | Bulgaria vs Lithuania | 1.62 | 3.74 | 5.69 |
| 19:15 | 5653 | The New Saints vs East Fife | 1.35 | 4.69 | 6.94 |
| 19:30 | 2131 | Peterhead vs Dundee Utd | 5.48 | 4.37 | 1.45 |
| 19:30 | 2747 | FC Cartagena vs Racing Santander | 2.37 | 2.97 | 3.02 |
| 19:30 | 5794 | Sporting Gijon vs Zaragoza | 2.24 | 2.88 | 3.37 |
| 20:00 | 3029 | Ivory Coast vs Morocco | 2.74 | 3.21 | 2.61 |
| 20:00 | 4523 | Rodina Moscow vs Akron Tolyatti | 2.18 | 3.28 | 2.88 |
| 21:00 | 1920 | Telstar vs Maastricht | 1.95 | 3.62 | 3.27 |
| 21:45 | 1447 | Hungary vs Serbia | 2.62 | 3.18 | 2.75 |
| 21:45 | 2371 | Italy vs Malta | 1.08 | 9.29 | 42.23 |
| 21:45 | 3653 | Denmark vs Kazakhstan | 1.18 | 6.74 | 15.79 |
| 22:00 | 2708 | Puerto Rico vs Guyana | 2.08 | 3.42 | 3.06 |
| 22:00 | 5660 | USA vs Germany | 3.65 | 3.80 | 1.91 |
| 22:00 | 5809 | Aruba vs Virgin Islands | U.s. | 1.18 | 6.11 |
| 22:00 | 5840 | Espanyol vs Valladolid | 2.05 | 3.32 | 3.32 |
| 22:30 | 3102 | La Luz FC vs Liverpool (URU) | 3.38 | 3.43 | 1.92 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 14, 2023

Nipashe



Rooney: Nitairejesha Birmingham Ligi Kuu UKURASA 21

# STARS YAPEWA NAFASI AFCON

## •••Ni baada ya kupangwa na Morocco, DRC na Zambia ambao...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya ratiba ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023) zitakazofanyika mwakani nchini Ivory Coast kutoka juzi, wadau wa soka nchini wameipa nafasi Timu ya Tanzania (Taifa Stars), ambayo itashiriki michuano hiyo kwa mara ya tatu.

Taifa Stars imepangwa Kundi F pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC)ambayo imetwaa ubingwa wa Afrika mara mbili (1968 na 1974), Morocco (1976), na Zambia ambayo ilichukua kombe hilo mwaka 2012 katika fainali zilizofanyika Gabon.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha wa zamani wa Taifa Stars, Charles Mkwasa alikiri Stars imewekwa kwenye kundi gumu, lakini akibainisha kama 'itachanga karata' zake vizuri inaweza 'kula sahani moja' na Wakongomani na Wazambia katika kusaka nafasi ya pili.

Mkwasa alisema kwake anaamini Morocco ina nafasi kubwa ya kumaliza ikiwa kinara katika kundi hilo, hivyo nchi tatu zilizobakia ndio zitapambana kusaka tiketi ya kusonga mbele.

"Kundi ni gumu, Morocco ni wazuri, Wakongo sasa hivi pia wamejipanga vizuri wamekuwa na kikosi bora, Zambia ni timu inayotupa tabu siku zote tangu miaka hiyo, kusema kweli siyo kundi la kufanyia masihara.

Morocco ni timu ambayo inaongoza kwa ubora Afrika kwa hiyo unaona kabisa nafasi yake ya kusonga mbele ipo, kinachosakwa hapo ni timu ya pili, sasa katika hizi timu tatu zilizobaki yoyote anaweza kwenda kama akijipanga vizuri," alisema Mkwasa.

Kocha na mchezaji huyo wa zamani wa Yanga alisema katika miaka ya karibuni kiwango cha DRC na Zambia kilishuka, lakini kwa sasa anawaona wamerejea kwenye ubora wao na itailazimu Taifa Stars kujipanga sawa sawa na hatimaye kuvuka hatua ya makundi.

"Kipindi cha nyuma Zambia alishuka kidogo uwezo na hata Jamhuri ya Kongo pia, naona kwa sasa zimejirekebisha, zimejipanga na ndiyo maana kwenye mechi za hivi karibuni zimekuwa zikifanya vyema. Zambia ina historia mbaya na sisi, mwaka 1979 tuliwatoa na tukaingia makundi kucheza AFCON ya 1980, leo tupo kundi moja, watakuwa waangalifu sana," Mkwasa alisema.

Alishauri kichaguliwe kikosi ambacho kitakuwa na wachezaji bora na wenye utimamu wa mwili na si wachezaji wanaokaa benchi kwenye klabu zao.

Kocha na mchezaji wa zamani wa Stars, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amewataka Watanzania kutoogopa na kuweka dhana ya timu

UKURASA. 23



Mshambuliaji nyota wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Simon Msuva. **PICHA: TFF**

# Simba SC, Yanga zachanga karata

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikiongeza 'dozi' ya mazoezi kwa wachezaji wake ili kujiandaa na mechi ya ufunguzi ya African Football League (AFL), dhidi ya Al Ahly kutoka Misri, watani zao Yanga wanaendelea kujiimarisha kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC utakaochezwa Oktoba 25, mwaka huu.

Simba itawakaribisha A Ahly katika mechi hiyo ya ufunguzi itakayofanyika Oktoba 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' aliliambia gazeti hili mbali na mazoezi ya uwanjani, ameanza kuwasoma wapinzani wao Al Ahly kwa kutizama picha za video za mechi walizocheza hivi karibuni kwa lengo la kufahamu ubora na madhaifu yao.

Robertinho alisema licha ya kikosi chake kutokamilika kutokana na baadhi kwenda kutumikia majukumu ya nchi zao, analazimika kuwapa mbinu nyota waliobakia huku watakapokamilika atafanya programu nyingine maalumu.

Alisema Al Ahly ni timu kubwa na yenye uzoefu wa kushiriki michuano mikubwa huku pia ikiwa na kikosi chenye wachezaji bora, hivyo wanajiimarisha ili kuwakabili kwa nguvu.

Kocha huyo alisema anaimani Simba pia ni wakubwa na wanaweza kupata matokeo mazuri katika mchezo huo na ule wa marudiano utakaochezwa Misri.

"Tumekuwa tukifanyia kazi mechi baada ya mechi, tulifanya vizuri mechi za ligi na sasa tunasuka kikosi chetu kuelekea mchezo dhidi ya Al Ahly, tunafahamu ubora wa wapinzani wetu lakini pia wana madhaifu yao.

Aliongeza mipango yake ni kuona Simba inaendelea kupata matokeo mazuri ikiwamo kushinda mechi ya ugenini dhidi ya Al Ahly.

Wakati huo huo Simba leo watazindua rasmi wiki ya hamasa

UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >